# WAKOLOSAI
# MTAALA

I. **MAELEZO KWA UJUMLA**.
   A. Mwalimu: Don Walker
   B. Mkalimani: Chris Mwakabanje
   C. Kila darasa linachukua takribani dakika 38.

II. **MAELEZO NA MALENGO**.
   A. Kujifunza kwa kina Waraka kwa Wakolosai.
   B. Mwanafunzi ataongeza ufahamu wake juu ya kanisa la Kristo na fursa ya kuzidishwa na Bwana ndani ya kanisa.
   C. Mwanafunzi atahamasika kuishi maisha yanayostahili jina analolivaa, yaani Mkristo.

III. **VIFAA MUHIMU WAKATI WA KUJIFUNZA**.
   A. Unapaswa uwe na vitu vifuatavyo:
      1. Biblia (swahili – UV, English – ASV, KJV, NKJV).
      2. Masomo katika kanda za video.
      3. Maelezo (Notes) au muhtasari wa kozi hii.

   B. Maoni: Tunapendekeza uwe na fafanuzi (commentary) yoyote yenye kushikilia mafundisho ya awali (conservative) katika Wakolosai.

IV. **MAMBO YA KUFANYA KATIKA KOZI HII**:
   A. Usome kitabu chote cha Wakolosai angalau mara tatu.
   B. Angalia kikamilifu kanda za video.
   C. Usome kikamilifu notisi zote za darasani.
   D. Kamilisha kazi yote ya kudondoa (maelezo hapo chini).
   E. Wasilisha makala ya muhula (maelezo hapo chini).
   F. Hakikisha unafanya mtihani mmoja mwishoni mwa kozi hii.
   G. Jumla ya maksi zako zinapaswa angalau kufikia asilimia 70.

V. **KAZI YA KUDONDOA**.
   A. Mistari ya kudodoa lazima iandikwe (au ichapwe) bila kutazamia mahali popote, kisha itumwe KBS kwa masahihisho. Mistari ni lazima itoke katika UV kama ulivyoonyeshwa katika fomu yako ya maombi ya kujiunga na KBS.

   B. Mistari yote ni sharti iandikwe ama kuchapwa katika mkao mmoja (mara moja). Unaweza kujifunza zaidi na kuandika upya mistari yote iwapo ulikosea, lakini unatakiwa kuanza upya yote na kuandikwa katika mkao mmoja.

   C. Katika kozi hii, mistari ifuatayo unapaswa kuidondoa:
      Wakolosa 1:18 — Wakolosai 2:9 — Wakolosai 2:14
      Wakolosai 3:16-21 — Wakolosai 4:6

   D. Kazi ya kudondoa uiwasilishe KBS wakati unatuma mtihani wako wa mwisho.

   E. Maoni: Njia bora ya kudondoa ni kuandika mistari katika vijikadi ili kwamba iwe rahisi kwako kuipitia mara kwa mara muda wote unaoendelea na kozi hii.

**VI. MITIHANI.**

A. Kuna mtihani mmoja wa kufanya katika Wakolosai.

B. Unapokaribia mwisho wa kitabu, wasiliana nasi na kuomba mtihani.

C. Ukishapokea mtihani, unaruhusiwa kuupitia na kujifunza.

D. Lakini, unapofanya mtihani, unatakiwa uufanye kikamilifu bila kutazama kwenye notisi, Biblia, kitabu, n.k.

**VII. MAKALA YA MUHULA.**

A. Andika makala juu ya muhtasari wa Wakolosai ukielezea mambo muhimu katika kila sura na kutoa masomo ambayo tunaweza kujifunza.

B. Makala inapaswa kuwa na kurasa nne, ikiwa imechapwa huku ukiruka nafasi mbili-mbili (double spaced). Ikiwa umeandika kwa mkono, makala isipungue kurasa sita, pasipo kuruka nafasi.

C. Makala itatakiwa unapotuma mtihani wako wa mwisho VBI pamoja na dondoa.

**VIII. MAKSI.**

A. Kazi ya kudondoa, makala ya muhula, na mtihani itasahihishwa tofauti tofauti.
B. Maksi za mwisho zitazingatia juu ya wastani wa kazi zako zote ulizopewa.
C. Unaweza kuomba ufafanuzi na kufikiriwa juu ya maksi, lakini iwavyo vyote KBS ndiyo itakuwa na uamuzi wa mwisho.

IX. **TUNZO**.

A. Tunzo itatolewa, ikiwa ni pamoja na cheti, pale tu utakapokuwa umefanikiwa kumaliza kazi yako kikamilifu, kanda za video umerejeza (kama uliziazima), na ada yote kwa kozi hii umelipa.

B. Mungu abariki jitihada yako ya kujifunza neno lake lenye uvuvio!

## SURA YA KWANZA

**Mstari wa 1**

A. Utume wa Paulo.
   1. Mdo.9:15 – "*Huyo ni chombo kiteule kwangu*."
      a. Mdo.22:21.

   2. 1 Kor.15:8-10; Gal.1:11-2:14.

   3. 2 Kor.12:11,12 hoja zenye kufikisha upeo wa juu wa hoja.

B. Timotheo (Timotheus).
   1. Mdo.16:1 – Mama, Myahudi aliyeamini; baba alikuwa Myunani.
   2. Mdo.16:2 – alishuhudiwa mema na ndugu wa Listra na Ikonia.
   3. 1 Kor.4:17 – Timotheo alitumwa Korintho.
      a. Katika 1 Kor.16:10,11 Paulo anawahamasisha Wakorintho wampokee Timotheo pasipo hofu miongoni mwao, na mtu awaye yote asimdharau.

        1) Inaonekana kwamba Timotheo alikuwa mwoga na mwenye aibu.
    4. Paulo alimsifia Timotheo.
        a. Flp.2:19 *"…Maana sina mtu mwingine mwenye nia moja nami, atakayeiangalia hali yenu*."
        b. 2 Tim.3:15.

**Mstari wa 2**

A. "*Kwa ndugu watakatifu waaminifu*."
    1. Watakatifu.
        a. Mtakatifu (hagios) wakfu, takaswa, kutengwa kando.
            1) Katika Agano Jipya linahusu tabia ya Mungu na mwenendo unaofanana na kulingana na namna alivyo.

        b. Law.11:44,47 – "*Utakuwa mtakatifu; kwa maana mimi ni mtakatifu…*" hubainisha tofauti kati ya kilicho kichafu na safi.

        c. 1 Pet.1:16.

        d. "*Kwa kanisa la Mungu lililoko Korintho, wale waliotakaswa katika Kristo Yesu, walioitwa wawe watakatifu pamoja na wote wanaoliitia jina la Bwna wetu Yesu Kristo kila mahali, Bwana wao na wetu*" (1 Kor.1:2).

        e. Mt.5:8; Yoh.15:19; 1 Tim.5:22.

    2. Ndugu waaminifu.
        a. Ebr.11:6; Yoh.8:24.
        b. 1 Kor.4:2; Ufu.2:10.
            1) Kutumaini na kuamini (trustworthy).

    3. "*Katika Kristo*."
        a. Gal.3:27; 1 Kor.12:13.
            1) 2 Tim.2:10; 1 Yoh.5:11; Rum.8:1; Ufu.14:13.
            2) Efe.1:3; Efe.1:1-14; 2:6.

    4. Neema na amani.
        a. Paulo anatumia salaam za kawaida kwa maana ya kuadhimisha.
            1) Sifa zenye kufuata desturi zimegeuzwa na mtume kuwa katika kuzitambua baraka zitokanazo na Ukristo.
                a) (*Charis*) – huruma asiyoistahili mtu.
                b) Palipo neema nyingi – amani hufuata.

            2) Asili ya neema na amani.
                a) "Kuna uthabiti mkubwa wa fikra sahihi kukubali asili ya baraka hizi. Baba ndiye 'Baba wa neema yote' (1 Pet.5:10)' na 'Mungu wa amani' (Ebr.13:20); na kwa kuzilinganisha na 'neema na kweli zilizoletwa kwa mkono wa Yesu Kristo"' (Yoh.1:17, naye 'ndiye amani yetu' (Efe.2:14). Bali Baba ndiye chimbuko na chemichemi ya baraka zote kwao waaminio." D. Lipscomb.

**Mstari wa3**

A. Shukrani kwa ndugu.
    1. Wala si suala la mtindo aliopenda kuutumia Paulo.

a. Kutotaja shukrani katika Wagalatia na 2 Wakorintho huonyesha palikuwa na kukua kiimani kwa upande wa waongofu wa Kolosai hata kustahili shukrani.

2. Kufurahia uadilifu wa watu wengine.
   a. Rum.12:15; 2 Yoh.4; 3 Yoh.4.
      1) Nitakuwa mkweli mimi mwenyewe – Math.5:16.
      2) Nitaachana na mambo yangu binafsi ikiwa yanamkosesha ndugu yangu – 1 Kor.8; Rum.14.
      3) Nitafanya kazi ya uinjilisti – Math.28; Mk.16; 2 tim.2:24.
      4) Nitajali na kuchapa kazi ya kuokoa kondoo zilizopotea – Lk.15.

B. Sala zilitolewa mbele za Mungu kupitia Yesu Kristo.
   1. Mt.6:9.
      a. Baadhi ya sala 26 Yesu alizotoa.
         1) Ingawa hatuna maneno yote katika sala hizo, kila sala iliyoandikwa inaonyesha mpangilio na inapelekwa mbele za Baba.
            a) Mt.11:25, 26; Yoh.12:28; Yoh.17.

      b. Mafundisho ya Yesu.
         1) Lk.11:1,2 Wanafunzi walimwomba Yesu awafundishe namna ya kusali. Alisema, "*Msalipo, semeni, Baba yetu uliye mbinguni*."

   2. Kusali kupitia kwa Kristo.
      a. Yoh.14:13, 14; 15:16.
      b. Ebr.7:25; Rum.8:34; 1 Yoh.2:1.
         1) Unamwomba Baba kwa njia ya Kristo Yesu.
            a) Ebr.10:19; 4:16.
            b) Yoh.16:20-22 – PIA ANGALIA mst. wa 23.

**Mstari wa 4**

A. Tangu waliposikia.
   1. Imani katika Kristo.
      a. Efe.1:15.
      b. Siyo imani tangulizi, bali imani inayodhihirika kwa kuishi kila siku kwa haki.
         1) Rum.1:17; Ebr.2:4.
         2) Gal.5:6; 1 Thes.1:3.
      c. Imani ilisikika kwa sababu iliweza kudhihirika kupitia matendo yao.

   2. "*Na upendo mlio nao kwa watakatifu wote*."
      a. Gal.5:22.
      b. 1 Pet.2:17; Yoh.15:12,13; 1 Kor.16:14.
      c. 1 Thes.1:3.
         1) Upendo huu unaweza kudhihirika, kwa sababu unaonekana kwa matendo.
            a) 1 Yoh.3:18.
            b) Ufu.3:19 (1 Pet.4:8; Yak.5:19,20).
            c) Upendo "kwa" ukionyesha mahali walikoudhihirisha huo upendo wao.

**Mstari wa 5**

A. "*Tumaini mliowekewa mbinguni*."
   1. Efe.1:18 "*Tumaini la wito wetu" na utajiri wa utukufu wa urithi*."

2. 1 Tim.1:1; Ebr.6:18.
   a) Ebr.9:24; Mdo.2; Ufu.3:21.
   b) Rum.8:24.

B. "*Mlizisikia*."
1. Rum.10:17; Yoh.20:30,31.

C. "*Neno la kweli ya injili*."
1. Umuhimu wa Neno la Mungu kwa wokovu.
   a. 1 Pet.1:23; Yoh.3:1-8.
   b. Yoh.6:63; Yak.1:21,22; Mdo.20:32.

2. Hebu angalia "*Neno*", "*Kweli*", na "*Injili*" yameunganishwa pamoja na kutajwa kama neno moja lenye kulenga maana moja.
   a. 2 Yoh.9; Yoh.15:1-8; 8:31,32.
   b. Kuna jambo litupasalo wote kulifanya, nalo kwa ufupi ni "*Neno la Kweli ya Injili*."

**Mstari wa 6**

A. Injili ilihubiriwa ulimwenguni kote.
1. Nukuu.
   a. Justin Martyr: "Hakuna watu wowote, Myunani au Mshenzi (Barbarian), au mwingine awaye yote…katika ujinga wote…ikiwa anakaa katika hema au anazunguka katika magari (wagon) yaliyofunikwa, ambapo sala na shukrani zake hazijatolewa kwa Baba Muumba wa viumbe vyote kupitia jina la Yesu aliyesulubiwa."

   b. Tertullian: "Sisi ni jana tu, lakini tayari tumejaza miji, visiwa, makambi, kasri yako, seneti, baraza. Tumekuachia tu mahekalu yako."

2. Maandiko:
   a. Mdo.19:10,20; 1 Thes.1:8; Flp.1:12; Rum.10:18.

B. Injili huzaa matunda.
1. Paulo anawaambia Wakolosai injili "*iliyofika kwenu*."
   a. Wazo katika Kiyunani ni "Kuwa karibu au kando yenu." Kenneth Wuest anaandika: "Dhana ni kwamba Injili imesogea karibu kabisa na watakatifu Wakolosai na wameipokea na kuihifadhi mioyoni mwao."

2. Rum.7:4; Yoh.15:1-8; 2 Pet.1:5-10; Gal.5:21,22.

C. Neema ya Mungu katika kweli.

**Mstari wa 7**

A. Epafra.
1. Hapa na 4:12,13; Flm.23.
   a. 1:7.
      1) Mjoli wetu mpendwa.
      2) Aliye mhudumu (servant) mwaminifu.

   b. 4:12,13.
      1) Kutoka Kolosai ("aliye mtu wa kwenu").

2) Akiomba daima kwa ajili yenu.
3) Kwa bidii kwa ajili yao.
4) Akiwahusisha pia wale walioko Laodokia na Hierapoli.

c. Film.23.
1. "*Aliyefungwa pamoja nami*."

B. "*Mhudumu mwaminifu*."
1. Lazima tutaje maneno ya Biblia kama vile Biblia inavyoyataja.

**Mstari wa 8**

A. "*Upendo katika Roho*."
1. Gal.5:22.
a. Si kwamba kila "upendo" ni sahihi.
1) 1 Yoh.2:15.
2) Kitabu cha Yeremia.
a) 2:2 – "upendo wa wakati wa uposo wako" – walimpenda Mungu.
b) 2:25 – "Nimewapenda wageni, nami nitawafuata."
c) 2:23 – "Jinsi ulivyoitengeneza njia yako ili kutafuta mapenzi?" Unatafuta mapenzi kokote kule isipokuwa kwa Yehova.
d) 5:31 – "Watu wangu wanapenda manabii wa uongo na kuchukuliana na makuhani."
e) 8:2 – "Mifupa…wataitawanya mbele ya jua, na mwezi, na jeshi lote la mbinguni, walivyovipenda."
f) 14:10 – "Bwana awaambia watu hawa hivi, hivyo ndivyo walivyopenda kutanga-tanga."
g) 31:3 – "Bwana alinitokea zamani, akisema, Naam nimekupenda kwa upendo wa milele, ndiyo maana nimekuvuta kwa fadhili zangu."

2. Bado, upendo wao ulikuwa "*katika roho*."
a. Mk.12:30.
b. 1 Pet.2:17.
c. 1 Yoh.3:18; 1 Thes.1:3.
d. Mt.5:43-48.

**Mstari wa 9**

A. "*Hatuachi kufanya maombi na dua kwa ajili yenu*."
1. Kuomba kwa niaba ya ndugu.
a. 1 Tim.2:1.
b. Flp.4:6; 1 Thes.5:17.

B. "*Kujaa maarifa ya mapenzi yake*."
1. Ni jambo la msingi kwamba Paulo anaomba ili wafahamu mapenzi ya Mungu.
a. Yak.1:21,22.
1) Mhu.12:13.
a) Tunatekeleza hili kwa kutenda mambo ambayo Mungu ametuamuru kufanya.

C. "*Katika hekima yote na ufahamu wa rohoni*."
1. Tena tunapaswa kuelewa tofauti hiyo ya hekima.
a. Yakobo 3:13-18.

        1) Kuna hekima ambayo "siyo ile ishukayo kutoka juu, bali ni ya duniani, ya tabia ya kibinadamu, na Shetani."

    b. Efe.5:17 – "Kwa sababu hiyo, msiwe wajinga…"
        1) Efe.4:18 – "Ambao; akili zao zimetiwa giza…kwa sababu ya ujinga uliomo ndani yao."

2. Hapo Paulo anasema, alitaka hekima na ufahamu wa "kiroho."
    a. Mafarisayo walijua jinsi ya kudanganya na kuwatawala kwa hila, hivyo basi wakamsulibisha Kristo.
    b. Lakini, wasingeelewa mambo ya kiroho.
        1) Math.13:13-15.

3. Lk.8:18 – "Jihadharini basi jinsi mnavyosikia."
    a. Kila mtu mmoja anatambua ni kiwango gani anaelewa ukweli kiroho.
        1) Kumbuka mifano.
            a) Math.7:7,8.

**Mstari wa 10**

A. "*Mwenende kama ulivyo wajibu wenu kwa Bwama*."
1. Maisha au mwenendo wa Mkristo mara nyingi umelinganishwa na jinsi ya kutembea (walk). Ni suala la utendaji.
    a. Efe.4:1 – "Mwenende kama unavyoustahili wito wenu mlioitiwa."
    b. Flp.1:27 – "Lakini mwenendo wenu na uwe kama inavyoipasa Injili ya Kristo."
    c. "1 Thes.2:12 – "Ili mwenende kama ilivyo wajibu wenu kwa Mungu, mwenye kuwaita ninyi ili mwingie katika ufalme wake na utukufu wake."
    d. 1 Thes.4:1 – jinsi iwapasavyo kuenenda na kumpendeza Mungu.
    e. 1 Yoh.2:6 – "imempasa kuenenda mwenyewe vile vile kama yeye alivyoenenda."

B. "*Mkizaa matunda kwa kila kazi njema*."
1. Math.7:15,21.
    a. Efe.5:11.
    b. Rum.7:4; Yoh.15:1-8; 2 Pet.1:5-10; Efe.2:8-10.

2. Angalia mtiririko wa matukio ambayo Paulo ameyaorodhesha kwa ajili yetu.
    a. Kwanza – maarifa, hekima, na ufahamu wa rohoni.
    b. Pili – Mwenendo wa Mkristo, tabia njema inayostahili.
    c. Tatu – Kuzaa matunda kwa kila kazi njema.

C. "*Na kuzidi katika maarifa ya Mungu*."
1. Hatua hizi tatu zitasababisha mtu kukua kiroho.
    a. "Maarifa."
        1) Hos.4:6; Isa.5:13.
        2) 2 Pet.3:18.
        3) Mdo.17:11; 2 Tim.2:15.

**Mstari wa 11**

A. "*Mkiwezeshwa kwa uwezo wote*."
1. Rum.1:16 – Efe.6:17 na Ebr.4:12.
2. 2 Kor.10:3-5.
3. Zab.10:7-11.

4. Mambo gani yatasaidia tukifahamu neno la Mungu.
   a. Rum.10:17 – Huzaa imani.
   b. Math.4:1-10 – Hutupatia silaha za kuyakabili majaribu; Zab.119:11.
   c. Mdo.20:32 – Hujenga / hutupatia urithi pamoja nao wote waliotakaswa.
   d. Yak.1:21 – Huokoa roho yako.
5. Walitakiwa kutiwa moyo ili kuweza kutimiza majukumu yao.
   a. Waweze kustahili majaribu (trials).
   b. Wayapinge wajaribu (temptation).
   c. Kutekeleza wajibu wao.
   d. Kuishi maisha ya imani.

B. "*Kwa kadiri ya nguvu za utukufu wake*."
1. Mungu ana uwezo wote (omnipotent).
   a. Efe.1:19-23.
      1) Mst.wa 19 "nguvu" (DUNAMIS) kwa kadiri ya utendaji (ENERGIA) wa nguvu (KRATOS) za uweza (ISCHUS) wake.

C. "*Saburi…uvumilivu pamoja na furaha*."
1. Saburi (HUPOMONE) – Saburi katika mtazamo wa vitu.
   a. Mtu aliyezingirwa na majaribu makubwa, huyastahimili, na wala havunjiki moyo au kupoteza lengo.
      1) Rum.5:3.
      2) 2 Kor.1:6.
   b. Kwa kifupi saburi hudhihirika kwa njia ya majaribu, taabu na dhiki.

2. Uvumilivu (MAKROTHUMIA) – Saburi katika mtazamo wa wanadamu.
   a. Mtu aliyewajeruhi wengine, hateseki mwenyewe kwa urahisi hata kukerwa na hao aliowakasirisha, au kuwapandisha hasira.

3. Furaha.
   a. Hatari ni hali ya kushindwa – hata ingawa tumedhihirisha saburi na uvumilivu – kwa majonzi au uchungu wa moyo.
   b. Tiba ni furaha ili kwamba Mkristo aweze kukabiliana na majaribu yote kwa hali ya uchangamfu mahiri.

**Mstari wa12**

A. "*Mkimshukuru Baba*."
1. 1 Zab.75:1.
2. 1 Kor.15:58; 2 Kor.2:14; 9:15.

B. "*Aliyewastahilisha kupokea*" (suitable).
1. Tunajadili hatua muhimu sana ya neno la Mungu.
   a. Efe.2:1-16.

2. Ilikuwa hatua kubwa hata manabii na malaika walitamani kuchungulia.
   a. 1 Pet.1:9-12.

C. "*Sehemu ya urithi wa watakatifu*."
1. Mdo.20:32.
2. 1 Pet.1:3,4; Rum.8:16,17.

D. “*Katika nuru*.”
   1. Yoh.1:4,5; 8:12.
   2. 1 Yoh.1:5-7.
   3. Efe.5:7-13.

**Mstari wa13**
A. “*Alituokoa kutoka nguvu za giza*.”
   1. Angalia maelezo katika mst.wa12.

B. “*Na kutuhamisha*.”
   1. Imetafsiriwa (METAHISTEMI) kubadilisha; kuondoa (META – yaani kugeuza, HISTEMI, kusababisha kusimama) hivyo basi, kuwezesha kusimama mahali pengine pa mageuzi.

C. “*Akatuingiza katika ufalme wa mwana wa pendo lake*.”
   1. Ebr.12:28,29; Math.16:16-19; Mdo.2.
   2. Ufu.1:5,9.
   3. Efe.5:27; 1 Kor.15:24.

**Mstari wa14**
A. “*Ambaye katika yeye tuna ukombozi*.”
   1. Ukombozi ni ndani ya Kristo Yesu.
      a. Rum.8:1; 2 Tim.2:10; 1 Yoh.5:11.

**UKOMBOZI**

A. Mambo matatu ya kuangalia kuhusu ukombozi:
   1. Kitu ambacho awali kilimilikiwa na mtu kisha kikapotea.
   2. Gharama zimelipwa ili kukirejeza upya.
   3. Nguvu zimevunjwa.

B. Hebu na tuyaangalie mambo hayo sasa.
   1. Kitu ambacho awali kilimilikiwa na mtu kisha kikapotea.
      a. Math.18:3; Isa.59:1,2.

   2. Lazima kulipia gharama, ili kukirejeza upya.
      a. 1 Pet.1:18,19; Efe.1:14; 1 Kor.6:19,20.

   3. Nguvu zimevunjwa.
      a. Mk.3:27; 1 Kor.15:55-57.

C. Damu.
   1. Ebr.9:22; 10:4.
   2. Isa.1:18; Zek.13:1.
      a. Mt.26:28; Kol.1:14; ufu.1:5; Rum.5:9; 3:24,25.

D. “*Msamaha wa dhambi*.”
   1. Haba.1:13; Isa.59:1,2.
      a. 2 Kor.5:21; Mk.15:34.
   2. Yer.3:25; Rum.6:23.

   a. Rum.3:10; 1 Yoh.1:8,10.

3. Mik.7:18,19; Isa.1:18.

**Mstari wa15**

A. "*Naye ni mfano wa Mungu asiyeonekana*."
   1. Yoh.1:1,14,18; 14:9.
   2. 2 Kor.4:4-6; Ebr.1:3.

B. "*Mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote*."
   1. Zab.89:27 – "Nami nitamjalia kuwa mzaliwa wangu wa kwanza, kuwa juu sana kuliko wafalme wa dunia."
   2. Ufu.3:14 – "…haya ndiyo anenayo yeye aliye Amina, Shahidi aliye mwaminifu na wa kweli, mwanzo wa kuumba kwa Mungu."
   3. Mashahidi wa Yehova huitaja mistari hii na kujaribu kuthibitisha kwamba Yesu Kristo ni kiumbe wa kwanza kuumbwa.
      a. Tafsiri (version) ya Ulimwengu (Kol.1:15-17). Angalia ndani ya Biblia hiyo.
         1) Yeye ni sura ya Mungu asiyeonekana, mzaliwa wa kwanza wa viumbe vyote; kwa sababu kwa njia yake vitu vyote [vingine] vilivyoumbwa mbinguni na duniani, vinavyoonekana na visivyoonekana, ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au serikali au mamlaka. Vitu [vingine] vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake. Pia, amekuwepo kabla ya vitu [vingine] vyote na vitu [vingine] vyote hushikamana katika yeye."

      b. Hata hivyo wamekuwa waaminifu vya kutosha katika "The Kingdom Interlinear Translation Of The Greek Scripture" hawajaongeza neno "vingine" ingawa neno hilo linapatikana katika tafsiri za Kiingereza.

      c. Katika mstari huu, neno linalojadiliwa ni "mzaliwa wa kwanza."
         1) Lakini, neno halimaanishi wakati wote mpangilio wa nyakati. Linaweza likamaanisha mwenye cheo kushinda wengine wote (preeminance).
            a) Chunguza mazingira kwa karibu, haswa mstari wa18.
            b) Kuna neno katika Kiyunani linaloonyesha kuumbwa kwanza na Paulo angeweza kulitumia hapa. Lakini hakulitumia.

      d. Sasa, hebu tuchanganue hitimisho (syllogism) kimantiki ambalo linakabili mafundisho ya Mashahidi wa Yehova, au kubainisha wazi utata wake.
         1) Kristo ndiye aliyeumba vitu vyote.
         2) Yeye mwenyewe ni kiumbe aliyeumbwa.
         3) Kristo alijiumba mwenyewe.

   4. Zaburi 89:27.
      a. Kama utaangalia tena mazingira, utaona panajadili kuwa na cheo kushinda wengine wote (preeminance).
      b. Angalia Zab.89:19 "Ndipo uliwaambia watakatifu wako kwa njozi [vision], ukasema, nimempa aliye hodari msaada; nimemtukuza aliyechanguliwa miongoni mwa watu."

   5. Ufu.3:14 – "Mwanzo wa kuumbwa kwa Mungu."
      a. Neno la Kiyunani haswa ni "aliyesababisha" (the cause) – aliyefanya viumbe vingine viwepo.

## UUNGU WA KRISTO

(Umilele wa Kristo)

A. Kutoka 3:14
   1. Mimi Niko" – hili lina asili moja sawa na lile la "Yehova."
      a. YHWH – Moja ya sifa yake ni wa milele.
      b. Kama tunaweza kuona kuwa "Yehova" limetumika likimlenga Kristo, basi yeye pia, ni wa milele.
         1) Isa.40:3.
            a) Mt.3:3; Mk.1:3; Lk.3:4; Yoh.1:23; Kut.6:3.
               1) Yesu = Bwana = YHWH = aliyekuwepo bila kusababishwa kuwepo.

   2. Isa.44:6; Ufu.1:17.

   3. Isa.44:24.
      a. Kol.1:16; Yoh.1:3.

   4. Yoh.1:1.
      a. "Kulikuwako" (was) limetokea mara tatu hapo.
         1) Kitenzi kisichotimilika (imperfect tense) – ni katika hali ya kwendelea.
         2) ICC anasema Daima Alikuwepo – (amekuwepo milele).

      b. Hivyo ingesomeka:
         1) "Hapo mwanzo daima kulikuwa na Neno, na Neno daima alikuwa kwa Mungu, na Neno daima lilikuwa Mungu."

   5. Yoh.17:5 – Kwa utukufu ambao daima nimekuwa nao.

   6. Kristo ni wa milele – Yeye ametangulia kabla ya viumbe vyote, na kama mzaliwa wa kwanza wa Mungu, ni mrithi wa yote.
      a. Ebr.1:2.

**Mstari wa16**

A. "*Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa*."
   1. Isa.44:24.
   2. Yoh.1:3 – "Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika."
   3. Ebr.1:2 – "Mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika Mwana aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu."

B. "*Vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka*."
   1. Kila kitu au kiumbe chochote kisicho Mungu kiliumbwa na Kristo.
      a. 1 Pet.3:22 – "Naye yuko mkono wa kuume wa kuume wa Mungu, amekwenda zake mbinguni, malaika na ezi na nguvu zikiisha kutiishwa chini yake."
      b. Kadhalika angalia Efe.1:21.

C. "*Vitu vyote viliumbwa kwa njia yake na kwa ajili yake*."
   1. Kumbuka mazingira.
      a. Kristo ana cheo kupita kila kitu.

**Mstari wa17**

A. "*Naye amekuwepo kabla ya vitu vyote*."
   1. Flp.2:6,7.

B. "*Na vitu vyote hushikamana katika yeye*."
   1. Yoh.1:10 – "Alikuweko ulimwenguni, hata kwa yeye ulimwengu ulipata kuwako, wala ulimwengu haukumtambua."
   2. Mdo.17:24 – "Mungu aliyeufanya ulimwengu na vitu vyote vilivyomo, yeye, kwa kuwa ni Bwana wa mbingu na nchi, hakai katika hekalu zilizojengwa kwa mikono."

**Mstari wa18**

A. "*Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika yote*."
   1. Katika Efe.1:21-23 Paulo anajadili kwa maelezo mengi mamlaka ya Kristo.
      a. Math.28:18.

   2. Mwili wa Kristo.
      a. Efe.1:22,23.
      b. Kuna mwili mmoja.
         1) 1 Kor.12:20; Efe.4:4.
         2) Math.16:18.

B. "*Naye ni mwanzo, mzaliwa wa kwanza katika wafu*."
   1. Rum.1:4; 1 Pet.1:3-4.
   2. 1 Kor.15:15-20.

C. "*Ili kwamba awe mtangulizi katika yote*."
   1. Maelezo haya hufikisha mwisho pointi zote za Paulo – Kristo ni mtangulizi (preeminent) katika yote.
      a. Kol.1:27; 2:10;3:1-3; 1-3; 2:11; 3:16,17.

**Mstari wa19**

A. "*Kwa kuwa katika yeye ilimpendeza* [Baba - KJ] *utimilifu wote ukae*."
   1. Kol.2:9; Yoh.1:14.
   2. Math.28:18-20.
   3. Flp.2:9-11.

**Mstari wa20**

A. "*Amani kwa damu ya msalaba wake*."
   1. Dhambi hututenganisha.
      a. Isa.59:1,2; Ebr.1:13.

   2. Tumekuwa karibu kwa njia ya damu ya Yesu.
      a. Efe.2:13.
         1) Efe.1:7; Kol.1:17.
         2) Damu huondoa tatizo la dhambi. Kwa hiyo wasioelewana wanaweza sasa kuwa na amani.
         3) Hili lilitekelezwa msalabani.
            a) 1 Kor.2:2.

B. Upatanisho.

1. 2 Kor.5:17-21; Rum.5:10; Efe.2:16.
2. Upatanisho.
   a. (KATALLASSO).
      1) Haswa likilenga kubadilika, kugeuza (fedha); kugeuka (binadamu) kutoka hali ya uadui na hata kufikia urafiki.

   b. (APOKATALLASSO).
      1) Muundo wenye kuonyesha mkazo zaidi.
      2) Kubadilisha kutoka hali moja na kuwa nyingine, ni kama kuondoa uadui wote hata kutosaza kizuizi chochote kwa umoja na amani.

C. "*Ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au vilivyo mbinguni*."
1. Efe.1:10 – "Yaani, kuleta madaraka ya wakati mkamilifu atavijumuisha vitu vyote katika Kristo, vitu vya mbinguni na vitu vya duniani pia. Naam, katika yeye huyo."
2. Ebr.1:3 akizungumzia juu ya Kristo "akivichukua vyote kwa amri ya uweza wake [by the word of His power), akisha kufanya utakaso wa dhambi."
   a. Angalia Ebr.11:39,40.

**Mstari wa21**

A. "*Na ninyi, …mlifarikishwa tena adui*."
1. Efe.2:1-3; Rum.6:17,18.
2. Rum.1:18-32.

B. "*Katika nia zenu, kwa matendo yenu mabaya*."
1. Rum.1:21,28.
2. Mk.7:18-23.
3. Efe.4:17-21.
4. Muda si mrefu au baadaye dhana ya nia itajadiliwa kwa vitendo.
5. 
6. 2 Kor.10:3-5.

C. "*Amewapatanisha sasa*."
1. Angalia maelezo katika mstari 20.
   a. Efe.2:1-10.

**Mstari wa22**

A. "*Katika mwili wa nyama yake, kwa kufa kwake*."
1. 1 Pet.2:24; 2 Kor.5:14-21; 1 Yoh.2:2; Efe.2:16.

B. "*Watakatifu, wasio na mawaa wala lawama*."
1. 1 Pet.1:13-17
   a. Tawala akili zako.
   b. Kuwa na kiasi.
   c. Tumaini.
   d. Utii.
   e. Kuwa mtu wa pekee.
   f. Mkimwiga Mungu.
   g. Hakuna kitu ambacho ni badala ya utakatifu.
   h. Kicho sahihi.
      1) Mhu.12:14; Kumb.5:20; Zab.89:7; 76:7,11; Ebr.10:31; Lk.12:5.

2. 1 Pet.2:9-12; Rum.12:1,2; Mdo.20:32; Flp.2:15-17.

**Mstari wa23**

A. "*Mkidumu tu*." (if - KJV)
   1. Neno lenye kuonyesha masharti.
      a. Kabla ya kupata matokeo, masharti lazima yatekelezwe.
         1) Yoh,.8:31; 2 Pet.1:5-10.

B. "*Mkidumu katika ile imani*."
   1. 1 Kor.15:58; Mk.10:22; Gal.6:9.
   2. Lk.8:12-15.

C. "*Msipogeuzwa na kuliacha tumaini la injili*."
   1. Kuanguka kutoka katika neema.
      a. 2 Pet.3:17; 1 Kor.10:12; Ebr.3:6; Ufu.2:10; Ufu.2:5,10; 3:5; 1 Kor.9:27; Gal.15:58; Yoh.15:2.

   2. Tumaini la Injili.
      a. Injili ndio hufunua tumaini.
         1) Rum.8:24.
         2) 1 Tim.1:1; Ebr.6:19,20; 1 Pet.1:3.

D. "*Mliyosikia*."
   1. Rum.10:14-17.

E. "*Iliyohubiriwa katika viumbe vyote vilivyo chini ya mbingu*."
   1. Angalia maelezo katika mstari 6.

F. "*Mimi Paulo nalikuwa mhudumu wake*."
   1. Ni jinsi gani Paulo anavyolitumia neno?

**Mstari 24**

A. "*Sasa nayafurahia mateso niliyonayo kwa ajili yenu*."
   1. Mateso na udhia haviepukiki.
      a. Flp.1:29; 2 Tim.3:12; 1 Pet.4:4.

   2. Mateso yenyewe hayana sura moja.
      a. Yanaweza kuwa mazuri au mabaya.
      b. Yanaweza kuleta mema au kuwa kikwazo.
         1) 1 Petro.
            a) 1:7-9.
            b) 4:12-16.

   3. Lazima tujifunze kufurahi katika mapambano.
      a. Mdo.5:41; Flp.4:4; Mdo.9:16; 2 Kor.12:9.

B. Kupata mateso kwa ajili ya kanisa.
   1. Flp.1:21-24; Efe.3:1,2; 2 Kor.11:28.
   2. Kwa kufanya hivyo, Paulo angeingia katika ushirika wa mateso ya Kristo.
      a. Flp.3:10.
         1) Upendo aliokuwa nao Kristo kwa kanisa ulisababisha mateso.

        2) Upendo aliokuwa nao Paulo kwa kanisa ulisababisha mateso.
        3) Je, unalipenda kanisa? – 1 Pet.2:17.

**Mstari wa 25**

A. "*Uwakili wa Mungu*."
  1. Uwakili – OIKONOMIA.
    a. Kimsingi ikilenga uongozi wa kaya (household).
        1) OIKOS – nyumba; NOMOS – sheria.
        2) Uwakili (stewardship).

    b. Hapa inarejea uwakili aliokabidhiwa "kutimiza neno la Mungu."
        1) Hilo ni kufunua mpango kamili wa Mungu na mzunguko wa habari za kweli zilizotimizwa katika kanisa ulio mwili wa Kristo. (W.E. Vine).
            a) Efe.3:8.
            b) 1 Kor.9:17,18.

**Mstari wa 26**

A. Ni huduma maalum ambayo inaunganishwa na siri ya Mungu.
  1. Ni makusudi ya Mungu hapo nyuma kuificha, lakini sasa kwa mapana hufunua na kudhihirisha kiutendaji kwa kupitia huduma ya Paulo [utumishi] ile ya kuwaingiza Mataifa katika imani sawa na ilivyokuwa kwa Wayahudi wanaoamini wakiwa washiriki wa urithi wa ahadi za Mungu na washiriki sawa wa mwili wa Kristo.

  2. 1 Tim.3:16; 1 Pet.1:10-12.
    a. Ilikuwa ni siri kubwa kwa manabii wa kale.
    b. Lakini, Yehova aliifunua kupitia watu hao aliowavuvia katika Kanisa karne ya kwanza.

**Mstari wa 27**

A. "*Mungu alipenda kuwajulisha siri*."
  1. Maneno yaliyoambatana na "siri."
    a. "Kuwajulisha", "kudhihirishwa", "kufunuliwa", "kuhubiriwa", kufahamika", na "uwakili,"

  2. Siri hii ni kubwa na inajumuisha vitu vingi.
    a. Kiini chake tunamwona Kristo (1:27).
    b. Kuwajumuisha Wayahudi na Mataifa ili kuwa wamoja (Efe.3:4-6).
    c. Ni mpango wa Mungu (Efe.1:9,10).

  3. Mambo haya yote yamefunuliwa katika Injili ya Yesu Kristo.

B. "*Utajiri wa utukufu wa siri hii*."
  1. Efe.1:8 – "Na utajiri wa utukufu wa urithi."
  2. Ingejulikana kwa Mataifa.

C. "*Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu*."
  1. Hilo ni hitimisho muhimu kwa ufupi.
    a. Kila jambo humlenga (centers) Kristo.

  2. Gal.2:20; Kol.3:16.

**Mstari wa 28**

A. "*Ambaye sisi tunamhubiri*."
   1. 1 Kor.2:2.
   2. Mdo.8:5, 12,35.
   3. Kila hotuba unayosoma katika kitabu cha Matendo  wazo lake kuu ni"Yesu Kristo."

B. "*Tukimwonya kila mtu*."
   1. Ezekieli 3 & 33 "Mlinzi."
   2. 2 Kor.5:11 – "Basi tukijua hofu ya Bwana, twawavuta wanadamu; lakini tumedhihirishwa mbele za Mungu. Nami natumaini ya kuwa tumedhihirishwa katika dhamiri zenu pia."
   3. Matendo 2:40.

C. "*Na kumfundisha kila mtu*."
   1. Mithali 1:1-7; 2:1-9.
   2. 2 Tim.2:2; Math.28:18ff.

D. "*Tupate kuleta kila mtu mkamilifu katika Kristo*."
   1. 2 Tim.3:16,17.
   2. Ebr.5:12-14.
   3. 1 Pet.2:2; 2 Pet.3:18.
   4. Zab.119:9-16.
   5. "*Katika Kristo*."

**Mstari wa 29**

A. "*Nami najitaabisha*."
   1. Efe.2:10.
   2. Flp.2:12,13.
      a. Majukumu ya wokovu.

## SURA YA PILI

**Mstari wa 1**

A. Jitihada kwa ajili ya Wakolosai, Walaodokia na watakatifu wote.
   1. Kuwajali kwake Paulo ndugu kumedhihirika kwa bidii yake ya kuchapa kazi na katika mapambano ya kiroho aliyokuwa nayo kwa ajili ya waongofu.

   2. Anawaandikia hao waliongolewa kupitia huduma yake pamoja na walifanya kazi pamoja naye.

   3. Angalia maelezo katika 1:24.

B. Laodokia Kol.4:16; Ufu.3:14ff.

C. Soma Kol.1:24-29.

**Mstari wa 2**

A. "*Ili wafarijiwe mioyo yao*."
   1. Maudhi yanakuja.
      a. 2 Tim.3:12; Flp.1:29; Mdo.9:16; 1 Pet.4:4.

   2. Mungu atawafariji.

a. 2 Kor.1:3,4 – “Na ahimidiwe Mungu, Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, Baba wa rehema, Mungu wa faraja yote; atufarijiye katika dhiki zetu zote ili nasi tupate kuwafariji wale walio katika dhiki za namna zote, kwa faraja hizo, tunazofarijiwa na Mungu.”

b. Zab.46:1; 1 Pet.5:7.

B. “*Wakiunganishwa katika upendo*.”

1. Yoh.15:12,13 – “Amri yangu ndiyo hii, Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi. Hakuna aliye na upendo mwingi kuliko huu, wa mtu kuutoa uhai wake kwa ajili ya rafiki zake.”

2. 1 Pet.2:17; 1 Kor.16:14.

3. 1 Pet.1:22 – “Mkiisha kujitakasa roho zenu kwa kuitii kweli, hata kuufikia upendano wa ndugu usio na unafiki, basi jitahidini kupendana kwa moyo.”

4. Ufu.3:19.

5. Upendo wa kweli wa Kibiblia utasababisha utendaji.
   a. 1 Yoh.3:18.

C. “*Wakapate utajiri wote wa kufahamu kwa hakika*.”

1. Ni wale tu ambao wangeupata utajiri kwa njia ya ufahamu wa ufunuo wa Mungu. Yaani, kupitia upendo wangepata utajiri ambao ungewaunganisha pamoja.

2. Paulo anarejea neno lile lile alilolitumia 1:27, pia katika 1:9, anapojadili utajiri mwingi wa maarifa.

D. “*Wapate kujua kabisa siri*.”

1. Upendo na ufahamu wa kweli huzaa matendo na imani. Huzalisha maarifa ya ukweli juu ya Mungu, na hivyo basi kuukiri ukweli huo.

2. Hulenga pia uwezo wa kutofautisha ukweli na uongo; mambo yaliyo ya kweli na yale yaliyo ya uongo.
   a. Ebr.5:12-14; 2 Yoh.9.

3. Kulikuwa na watu walionena elimu kama ndiyo mwisho wa yote. Neno la Kiyunani, GNOSIS, humaanisha maarifa.
   a. Ufunuo, hata hivyo, hauwezi kueleka vyema mbali na kuuchimba upendano wa ndugu.
   b. Efe.3:17-19.

E. Juu ya Mungu, na juu ya Baba, na juu ya Kristo.

1. Siri, kiini chake ni katika Yehovah.
   a. Efe.3:9-11.
   b. Angalia 1:27.

**Mstari wa 3**

A. “*Ambaye ndani yake yeye hazina zote za hekima na maarifa zimesitirika*.”

1. Ndani ya Kristo.
   a. Rum.8:1; 2 Tim.2:10; 1 Yoh.5:11; Ufu.14:13; Efe.1:3.

    b. Mistari ya awali kumi na minne ya Waefeso sura 1 hujadili kwa mapana baraka zipatikanazo "ndani ya Kristo."
    c. Gal.3:27.
2. Hazina ya hekima na maarifa.
    a. Ni lazima tuelewe thamani ya neno la Mungu na mambo linayoweza kutimiza.
        1) Yak.1:21; Mdo.20:32; Rum.1:16; Zab.119:9,9; 130.

3. Hekima, maarifa, na busara.
    a. Hekima hutegemea elimu (knowledge). Busara ni jinsi ya kuitumia hekima.

4. Mambo hayo yote ambayo yana thamani kwa mtu hupatikana ndani ya Kristo.

**Mstari wa 4**

A. Mtu asije akawadanganya kwa maneno ya kuwashawishi.
1. Rum.16:17,18 – "Ndugu zangu, nawasihi, wangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume cha mafundisho mliyojifunza; mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza waidanganya mioyo ya watu wanyofu."

2. 2 Timotheo 3.
    a. Mistari 1-5, Paulo anajadili nyakati za hatari zitakazokuja.
    b. Katika mistari 6,7 anasema, "Kwa maana katika hao wamo wale wajiingizao katika nyumba za watu, na kuchukua mateka wanawake wajinga wenye mizigo ya dhambi, waliochukuliwa na tamaa za namna nyingi; wakijifunza siku zote, ila wasiweze kabisa kuufikia ujuzi wa kweli."

3. Tito 1:10 – "Kwa maana kuna wengi wasiotii wenye maneno yasiyo na maana, wadanganyaji, na hasa wale wa tohara, ambao yapasa wazibwe vinywa vyao."

4. 2 Pet.2:3 – "Na katika kutamani watajipatia faida kwenu kwa maneno yaliotungwa ambao hukumu yao tangu zamani haikawii, wala uvunjivu wao hausinzii."

**Mstari wa 5**

A. "*Maana nijapokuwa sipo kwa mwili, lakini nipo pamoja nanyi kwa roho*."
1. Ingawa Paulo alikuwa mbali nao kimwili, akili zake zilikumbuka daima juu ya masuala yao ya kiroho na kukua kwao.

B. "*Nikifurahi na kuuona utaratibu wenu na uthabiti wa imani yenu katika Kristo*."
1. Sifa njema kutoka kwao zilimfanya Paulo ajisikie furaha. Walikuwa imara katika imani.
    a. 1 Kor.15:58; Uf.2:10.

2. Tofauti zinazovutia kuzifahamu.
    a. Katika 1 Kor.5:3-5 – Watu aliowajua vema Paulo. Alichukizwa nao, akiwa pamoja nao katika roho, aliwakemea kwa kushindwa kwao kukemea dhambi kambini.
    b. Kwa mazingira hayo, ingawa Paulo hakuwepo kimwili bali kiroho, alipata fursa ya kufurahi , na hao ni watu ambao hakuwahi kukutana nao.

**Mstari wa 6**

A. "*Basi kama mlivyompokea Kristo Yesu, Bwana."*
1. Waliipokea injili na kuitii.

2. Walidumu kuwa imara katika imani (2:5).
   a. 1:4-6.

3. Changamoto zilikuwa zinawajia mbele yao.
   a. 2:4,814ff.

B. *"Enendeni vivyo hivyo*."
   1. Endeleeni, kuwa imara.
      a. 1 Yoh.1:7; Efe.5:2.
      b. Efe.4:17 "Msienende kama Mataifa waenendavyo."

**Mstari wa 7**

A. "*Wenye shina na wenye kujengwa katika yeye*."
   1. Lk.8:13 – "Na wale penye mwamba ndio wale ambao wasikiapo hulipokea lile neno kwa furaha; nao hawana mizizi, huamini kitambo kidogo, na wakati wa kujaribiwa hujitenga."
      a. Wakolosai hawa walilisikia neno, na kulipokea kwa furaha.
         1) Aliwataka wawe na shina pamoja na kukua.

   2. Zab.1:1-3 – "Heri mtu yule asiyekwenda katika shauri la wasio haki; wala hakusimama katika njia ya wakosaji; wala hakuketi barazani pa wenye mizaha. Bali sheria ya Bwana ndiyo impendezayo, na sheria yake huitafakari mchana na usiku. Naye atakuwa kama mti uliopandwa kandokando ya vijito vya maji, uzaao matunda yake kwa majira yake, wala jani lake halinyauki; na kila alitendalo litafanikiwa."

B. "*Mmefanywa imara kwa imani*."
   1. Kufanywa imara.
      a. Rum.16:25,27 – "Sasa na atukuzwe yeye awezaye kuwafanya imara, sawasawa na injili yangu…Ndiye Mungu mwenye hekima yote. Utukufu una yeye kwa Yesu Kristo milele na milele. Amina.

      b. 1 Thes.3:13 – "Apate kuifanya imara mioyo yenu iwe bila lawana katika utakatifu mbele za Mungu, Baba yetu, wakati wa kuja kwake Bwana wetu pamoja na watakatifu wake wote."

      c. 2 Thes.2:16,17 – "Na Bwana wetu Yesu Kristo mwenyewe, na Mungu Baba yetu, aliyetupenda akatupa faraja ya milele na tumaini jema, katika neema, awafariji mioyo yenu, na kuwafanya imara katika kila neno na tendo jema."

      d. 2 Thes.3:3 – "Lakini Bwana ni mwaminifu, atakayewafanya imara na kuwalinda na yule mwovu."

      e. Yak.5:8 – "Nanyi vumilieni, mthibitishe mioyo yenu, kwa maana kuja kwake Bwana kunakaribia."

      f. 1 Pet.5:10 – "Na Mungu wa neema yote aliyewaita kuingia katika utukufu wake wa milele katika Kristo, mkiisha kuteswa kwa muda kidogo, yeye mwenyewe atawategemeza, na kuwathibitisha, hata milele na milele. Amina."

   2. Paulo alitaka zaidi, Wakristo wabakie kuwa waaminifu.
      Katika sura ya 2, anatoa tahadhari ya hatari na kuwaonya Wakristo kubakia kuwa waaminifu.
         1) Kwa njia ya neno.

a) Yoh.8:31,32; Tito 1:9; 1 Pet.3:15; Yuda 3.

2) Kwa njia ya upendo.
a) 1 Kor.16:14; Rum.12:9,10; 1 Yoh.3:18; 1 Pet.2:17.

C. Kama mlivyofundishwa.
1. Math.28:18ff.
2. 2 Tim.2:2.

D. Mkizidi kutoa shukrani.
1. Zab.75:1.
2. Flp.4:6.
3. 1 Thes.5:18 – "Shukurani kwa kila jambo; maana hayo ni mapenzi ya Mungu kwenu katika Kristo Yesu."
4. 1 Kor.15:57; 2 Kor.2:14.

**Mstari wa 8**

A. Jiangalieni.
1. (Kiyunani – PROSECHO) Kuzingatia akilini, k.m. kuwa makini, jihadhari, kuwa mwangalifu mwenyewe, shikilia ahadi.
a. Math.7:15 – "Jihadharini na manabii wa uongo wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali."

b. Math.10:17 – "Jihadharini na wanadamu; kwa maana watawapeleka mabarazani, na katika masinagogi yao watawapiga."

c. Math.16:6 – "Yesu akawaambia, angalieni, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo."

2. (Kiyunani – BLEPO) – Tazama, jiangalieni, tambua, zingatia, jihadharini.
a. Mk.8:15 – "Akawaagiza, akasema, angalieni, jihadharini na chachu ya Mafarisayo na chachu ya Herode."
b. Mk.12:38 – "Akawaambia katika mafundisho yake, jihadharini na waandishi, wapendao kutembea wamevaa mavazi marefu, na kusalimia masokoni."
c. Flp.3:2 – "Jihadharini na mbwa, jihadharini na watendao mabaya, jihadharini na wajikatao."
1) Ni neno hili la Kiyunani BLEPO, linalopatikana katika Kol.2:8.

B. "*Asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo*."
1. Angalia nukuu hii kutoka kwa David Lipscomb:
a. "Falsafa zote za wanadamu, udanganyifu wote wa hekima za wanadamu, na ufidhuli wa ulimwengu wenye kubuniwa pamoja na fikra za wanadamu huwateka watu, huangamiza nafsi zao, huwapeleka katika mauti ya milele kwa kuwatenga mbali na Mungu pamoja na wokovu wake."

b. "*Mateka*" - Kutwaliwa kama nyara, kuchukuliwa kama mateka wa vita, kutwaliwa kama watumwa.

c. "*Elimu*" – (Kiyunani – PHILOSOPHIA).
1) Tunaona hapa tu katika Agano Jipya.
2) Kutafuta (pursuit) hekima.

3) Mdo.17:18 (Kiyunani – PHILOSOPHOS) KUPENDA HEKIMA.
4) Yak.3:13-18.
   a) Mithali 1:2; 2:4.
   b) Hapa inawezekana inalenga hekima ya dunia.

d. "*Madanganyo matupu*" – Kwa hila au ujanja.

C. "*Kwa jinsi ya mapokeo*."
1. 2 Thes.2:15, 3:6 – Kuna mapokeo mazuri kutoka kwa Mungu.
2. Mk.7:3 – Hapa anazungumzia mapokeo mabaya mfano Kol.2:8.

D. "*Kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu*."
1. Gal.4:3 – "Tulikuwa tukitumikishwa na kawaida za kwanza za dunia."
   a. Mazingira ndiyo hutoa maana ya kuelewa mambo ya ulimwengu kuwa ni masuala ya Kiyahudi.
   b. Angalia Gal.3:24-29.

2. Lakini, mazingira yetu katika Kolosai 2 ni masuala ya ufedhuli wa upagani.
   a. Hili ndilo hasa Paulo analolijadili katika mazingira haya.

E. "*Wala si kwa jinsi ya Kristo*."
1. Hapa ndio tunaona ufunguo wa mstari huu.
   a. Yoh.8:31, 2 Yoh.9.
   b. Walikuwa wameyaacha mafundisho ya Kristo, au walikuwa wakijaribu kuyaweka pembeni mafundisho ya Kristo, wakiyaendea mafundisho, mapokeo na hekima za wanadamu za ulimwengu. Hili haswa ndilo Paulo anawaonya.

**Mstari wa 9**

A. "*Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili*."
1. Kol.1:19.
2. Palikuwa na mmoja aliyeshiriki kikamilifu asili ya Mungu, akafanyika mwili akakaa katika nyumba ya maskani akiwa miongoni mwa wanadamu.
   a. Yoh.1:1-3,14.
3. Bila yeye, Kristo, hatujakamilika kabisa.
4. Lakini tukiungana naye, tukishirikiana naye, na kujikuta katika kifungo cha kuishi pamoja naye, katika yeye tunaheshima sisi kwa sisi, mfano wa mwili na kichwa.
   a. Efe.1:23; Yoh.1:16; Flp.2:12,13; Efe.2:10.

B. "*Utimilifu wote wa Mungu*" – (Godhead)
1. Mdo.17:29 – "Basi, kwa kuwa sisi tu wazao wa Mungu, haitupasi kudhani ya kuwa Uungu ni mfano wa dhahabu au fedha au jiwe, vitu vilivyochongwa kwa ustadi na akili za wanadamu."

2. Rum.1:20 – "Kwa sababu mambo yake yasiyoonekana tangu kuumbwa ulimwengu yanaonekana, na kufahamika kwa kazi zake; yaani, uweza wake wa milele na Uungu wake; hata wasiwe na udhuru."
   a. (Kiyunani – THEIOS) – Divine Godhead.

3. Kol.2:9.
   a. (Kiyunani – THEOTES) – Godhead.

4. Maneno yote mawili yametoka katika shina moja.
    a. (Kiyunani – THEOS) – (Deity, the supreme divinity) – Mungu.

C. Kimwili.
  1. Yoh.14:9-11, "Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, utuonyeshe Baba? Husadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu? Hayo maneno niwaambiayo mimi siyasemi kwa shauri langu; lakini Baba akaaye ndani yangu huzifanya kazi zake. Mnisadiki ya kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yu ndani yangu; la! Hamsadiki hivyo, sadikini kwa sababu ya kazi zenyewe."

**Mstari wa 10**

A. "*Na ninyi mmetimilika katika yeye*."
  1. Yoh.8:36 – "Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli."

  2. Yoh.4:14 – "Lakini ye yote atakayekunywa maji yale nitakayompa mimi hataona kiu milele; bali yale maji nitakayompa yatakuwa ndani yake chemchemi ya maji, yakibubujika uzima wa milele."

  3. Flp.4:19 – "Na Mungu wangu atawajazeni kila mnachokihitaji kwa kadiri ya utajiri wake, katika utukufu ndani ya Kristio Yesu."

B. "*Kichwa cha enzi yote na mamlaka*."
  1. Math.28:18.
  2. Kol.1:15-18 – Ukuu wake Kristo umetiliwa mkazo kuwa yu juu ya vitu vyote.

**Mstari wa 11**

A. "*Mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono*."
  1. Rum.2:25-29.

  2. Gal.2:7.
      a. Lk.2:21 – Wayahudi walitahiriwa siku ya nane.

  3. Lakini huu ni tofauti.
      a. Lk.9:23.
      b. Ebr.12:1,2.
      c. Gal.5:16-21.

  4. Ni maana ya kiroho ya kuvua utu wa kale uliotajwa hapa.

B. Kwa kuuvua mwili wa dhambi.
  1. Efe.4:22-24.
  2. Rum.6.

**Mstari wa 12**

A. "*Mkazikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo*."
  1. Rum.6:3,4.

B. Mmefufuliwa.
  1. Rum.6:3,4.

        a. 2 Kor.5:17.

C. Kuamini katika nguvu zake Mungu.
    1. Imani – ninaweza kuitambua.
        a. Rum.10:17; Yoh.20:30,31.

    2. Nguvu zake Mungu.
        a. Si za mwanadamu bali Mungu.

    3. Ni jinsi gani Mungu anafanya kazi?
        a. Math.26:28; Mdo.2:38.
        b. Ufu.1:5; Mdo.22:16.
        c. Rum.6:3,4.

D. Ni nani aliyemfufua Kristo kutoka kwa wafu?
    1. Efe.1:19-2:10.
    2. Rum.1:4.
    3. 1 Pet.1:3-5.

E. Swali: Je, ubatizo ni muhimu?
    1. Gal.3:27; Lk.16:16; Yoh.3:5; Mdo.22:16; 2:38; Mdo.8; Rum.6:3,4.

**Mstari wa 13**

A. "*Mlikuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu*."
    1. 1 Tim.5:6; Ufu.3:1.

    2. Math.8:22 – "Lakini Yesu akamwambia nifuate; waache wafu wazike wafu wao."

    3. Lk.15:24,32 – "Kwa kuwa huyu mwanangu alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana. Wakaanza kushangilia." Mst.wa 32 "Tena kufanya furaha na shangwe ilipasa kwa kuwa huyu ndugu yako alikuwa amekufa, naye amefufuka; alikuwa amepotea, naye ameonekana."

    4. Rum.6:23.

    5. Isa.59:1,2.

B. "*Aliwafanya hai pamoja naye*."
    1. Kol.3:1.

    2. Maneno hayo haswa yanamaanisha "Nanyi amewawezesha kuishi pamoja naye."
        a. Yoh.5:21; Rum.4:17.
        b. Yoh.10:10; 14:6.

    3. "Nguvu ile ile iliyotenda kazi juu ya mwili wa Yesu uliokufa, na kumfufua kutoka kwa wafu hata kumwinua juu kabisa kwa kumketisha kitini mkono wa kuume wa Mungu, inatenda kazi juu yao waliokufa kwa makosa na dhambi, kushiriki kwa njia ya imani utukufu wa uzima wa milele." David Lipscomb uk. 38.

C. "*Akiisha kutusamehe makosa yote*."
    1. Efe.1:7; Kol.1:14.

2. Mik.7:18,19.
3. Isa.1:18 – “Haya, njooni, tusemezane, asema Bwana, dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; zijapokuwa nyekundu kama bendera; zitakuwa kama sufu.”

**Mstari wa 14**

A. Paulo sasa anasisitiza kwa hao waalimu wa uongo wote. Waliitafuta hekima ya dunia na maarifa, na kuwashutisha ndugu hao. Sasa anaibainisha sheria ya Musa, sheria ambayo isingeleta msamaha.
   1. Andiko au maagizo.
      1. Efe.2:15.
         a. Hapa rejea ni katika sheria ya kale.

      2. Lakini kwa nini sheria ya kale iliondolewa?
         a. Haikuweza kumsaidia mwanadamu na unyonge wake.
         b. Rum.7.
         c. Ebr.10:4.

      3. Hivyo basi ilikuwa kinyume nasi.
         a. Iliweza kuibainisha dhambi, iliionya dhambi, lakini (Agano la Kale) halikuweza kutatua tatizo la dhambi lenyewe kikamilifu.

B. Hivyo basi ilikuwa kinyume nasi.
   1. Gal.3:19.
      a. Ilionyesha tatizo.
      b. Lakini haikuwa na tiba ya tatizo.
         1) 2 Kor.3:6-11.

C. Akaipigilia msalabani.
   1. Mdo.15:10,11 – “Basi sasa mbona mnamjaribu Mungu na kuweka kongwa juu ya shingo za wanafunzi, ambalo baba zetu wala sisi hatukuweza kulichukua. Bali twaamini kwamba tutaokoka kwa neema ya Bwana Yesu vile vile kama wao.”

   2. Gal.3:10 – “Kwa maana wale wote walio wa matendo ya sheria, wako chini ya laana; maana imeandikwa, amelaaniwa kila mtu asiyedumu katika yote yaliyoandikwa katika kitabu cha torati, ayafanye.”

   3. Rum.6:14 – “Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi; kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.”

   4. Gal.3:19-25.

   5. Ebr.5:6-13.

   6. Yoh.19:30 – “Imekwisha.”

**Mstari 15**

A. “*Akiisha kuzivua enzi na mamlaka*.”
   1. Enzi na mamlaka.
      a. Tito 3:1 – “Uwakumbushe watu kunyenyekea kwa wenye uwezo na mamlaka, na kutii, na kuwa tayari kwa kila kazi njema.”

1) Rum.13:1 – "Kila mtu na aitii mamlaka iliyo kuu; kwa maana hakuna mamlaka isiyotoka kwa Mungu; na ile iliyopo imeamuriwa na Mungu."
2) 1 Pet.2:13 – "Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana; ikiwa ni mfalme kama mwenye cheo kikubwa."

b. Rum.8:38 – "Kwa maana nimekwisha kujua hakika ya kwamba, wala mauti, wala uzima, wala malaika, wala wenye mamlaka, wala yaliyopo, wala yatakayokuwepo, wala wenye uwezo."

c. "Efe.3:10 – "Ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwenugu wa roho."

d. Efe.6:12 – "Kwa maana kushindana kwetu si juu ya damu na nyama, bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho."

e. Kol.1:16 – "Kwa kuwa katika yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi, au usultani, au enzi, au mamlaka; vitu vyote viliumbwa kwa njia yake, na kwa ajili yake."

f. Efe.1:21 – "Juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia."

g. Kol.2:10 – "Na ninyi mmetimilika katika yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka."

2. Mitazamo mbalimbali.
 a. F.F. Bruce katika "The New International Commentary on the New Testament – "Ametiisha enzi zote ambazo zilituhukumu kwa kutuweka chini ya himaya zake. Kifaa kile kile cha fedheha na mauti ambacho nguvu za maadui walidhania kuwa wameweza kukitumia na kumshinda yeye milele kiligeuzwa naye kuwa kifaa cha kushindia na kuwafanya mateka.

 b. The New Bible Commentary – "Maadui hapa ni enzi na mamlaka za kiroho – ambazo hata hivyo zimesalimisha na kuweka silaha chini k.m. kunyang'anywa na kutokuwa na nafasi tena ya kutuangamiza."

 c. Kenneth Wuest – Wuest Word Studies On Ephesians and Colossians. "Falme na mamlaka ni sawa na Efe.6:12 – jeshi la Shetani katika mazingira ya ulimwengu huu.

 d. The Expositors Bible Commentary. Vol 11 – "Tafsiri inayoshabihiana ni ile inayoonyesha uadui wa uweza wa kimiujiza kiroho. Utawala mwovu. Maneno yenye kuunganisha mamlaka zote za ulimwengu huu ambazo zinamwasi Mungu, mahali pengine zikitajwa kama 'Wakuu wa ulimwengu huu wa giza' (Efe.6:12; linga. Kol.1:16, 2:8, 19)."

 e. David Lipscomp – "Hii ni taswira inayotokana na jinsi maadui walivyotendewa waliposhindwa. Yesu alihukumiwa na kuuawa na wafalme na wakuu wa serikali za ulimwengu huu – Wayahudi na Warumi.

 f. Burton Coffman – "Hawa hujulikana kama watu wenye cheo katika jamii ya wakuu wa Wakiyahudi Yerusalem. Kadhalika ukimjumuisha pengine na liwali wa Rumi katika siku za Paulo alipokuwa tayari kapokea adhabu kali kama vile inavyoelezwa 'Aliteseka chini ya Pontio Pilato.'"

B. “*Akazifanya mkogo*.”
   1. Ufu.1:18.

C. Akazishangilia.
   1. Msalaba ndicho chombo cha ushindi dhidi ya nguvu hizo mbaya.

   2. Ufufuo.
      a. 1 Kor.15.
      b. Rum.1:4.
      c. Huu ndio ushindi wa Kristo.

   3. Ni shangwe kamili.
      a. Yoh.12:30-32; Tito 2:14; Math.12:29; 25:41; Ebr.2:14.

**Mstari wa 16**

A. “*Basi, mtu asiwahukumu*.”
   1. Kuna kipimo cha hukumu.
      a. Yoh.12:48.
      b. Yoh.7:24.

   2. Kol.2:14; Ebr.8.
      a. Sheria ya kale, pamoja na sheria za vyakula mbalimbali, sikukuu, na siku takatifu, haya si kipimo cha hukumu.

B. Vyakula na vinywaji.
   1. Sheria za vyakula za Agano la Kale ziligongomelewa na Kristo msalabani.
      a. 1 Kor.8:1; Rum.14:1-3; 1 Kor.10:23-25.

C. Katika kuangalia sikukuu.
   1. Hes.10:10; 28:11.
   2. 1 Nyak.23:31 – “Na kumtolea BWANA sadaka zote za kuteketezwa, katika siku za sabato, za mwezi mpya, na za sikukuu zilizoagizwa, idadi kulingana na agizo lake, siku zote mbele za BWANA.”

D. Sabato.
   1. Ikimaanisha kupumzika au kustarehe.
      a. Kivuli cha mapumziko ya waumini wanaoupata ndani ya Kristo.
         1) Ebr.4:3-11.

      b. Mungu alipumzika katika kazi zake zote.
         1) Iliingizwa katika utaratibu wa Musa.
            a) Kutoka 20:8-11; Kumb.5:12-15.

   2. Haijaingizwa, hata hivyo, katika Agano la Kristo.

**Mstari wa 17**

A. “*Kivuli cha mambo yajayo*.”
   1. Ebr.10:1.
   2. Gal.3:24,25.

B. Mwili ni wa Kristo.
    1. Math.26:28 dhidi ya Ebr.10:4.

    2. Ebr.8:5 – "Watumikiao mfano na kivuli cha mambo ya mbinguni, kama Musa alivyoagizwa na Mungu alipokuwa tayari kuifanya ile hema maana asema, Angalia ukavifanye vitu vyote kwa mfano ule ulioonyeshwa katika mlima."

**Mstari 18**

A. "*Mtu asiwanyang'anye* [beguile] *thawabu*."
    1. Kudanganya (Beguile – PARTABRABEUO), kutoa thawabu isiyo yenyewe, kulaghai (wokovu), kughilibu wokovu.
        a. Kol.2:4.
            1) (Kiyunani PARALOGIZOMAI), kushindwa kutambua, kudanganywa, kulaghaiwa, au kughilibiwa.

        b. 2 Kor.11:3.

        c. Vincent anasema: "Tabia za waalimu wa uongo inahusisha kuketi hukumuni kama watoao thawabu kwao waliokana mafundisho yao ya kutafakari malaika. Paulo ananena hivyo kulingana na mtazamo wao."

B. "*Kwa kunyenyekea kwa mapenzi yake mwenyewe tu, na kuabudu malaika*."
    1. Unyenyekevu ni jambo linalotakiwa.
        a. Flp.1:3,4; Yak.4:10.
        b. 1 Pet.5:5,6.
        c. Obad.3; Mith.16:18.

    2. Lakini, unyenyekevu wa mapenzi yao katika kuabudu malaika.
        a. Lazima uelewe mtazamo wa "Gnostic."
            1. Tunajadili juu ya unyenyekevu juu ya uongo au "ulio zaidi."

            2. Ibada ya malaika.
                a. Math.4:14.
                b. Ebr.1:5; Ufu.19:10.
                    1) Pia ukijumuisha huduma ya upatanisho wa malaika.
                        a) 1 Tim.1:2-5.
                c. Wuest anasema: "Kuabudu malaika ni kuonyesha unyenyekevu, upendo wenye kicho kingi kwa Mungu, kama inavyodhihirika katika kujaribu kupinga kumwendea Mungu kwa njia ya moja kwa moja: katika dhana ya kwamba unyenyekevu, kujidhili hata kutoshika vitu, lazima basi kumfika mbele za Mungu kwa kupitia msururu wa madaraja ya viumbe vya kati."

C. Vitu ambavyo mwanadamu hajaviona.
    1. Hawajui mambo ambayo wanayazungumza.

D. Kujivuna katika akili zao za mwili.
    1. Hili linaonyesha unyenyekevu huo kuwa sio sahihi.

**Mstari wa 19**

A. “*Wala hakishiki kichwa*.”
   1. Waalimu wa uongo wamepoteza mawasiliano na Kristo.
      a. 2:10; Kol.1:18.

B. “*Ukiruzukiwa na kuungamanishwa*.”
   1. Efe.3:21.
   2. Efe.1:1-14.
   3. 2 Tim.2:10; 1 Yoh.5:11.
   4. Efe.1:22,23.

**Mstari wa 20**

A. “*Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo*.”
   1. Rum.6:1-4; Gal.2:20.

   2. 2 Kor.4:10 – “Siku zote twachukua katika mwili kuuawa kwake Yesu, ili uzima wa Yesu nao udhihirishwe katika miili yetu.”

   3. 2 Tim.2:11 – “Ni neno la kuaminiwa. Kwa maana kama tukifa pamoja naye, tutaishi pamoja naye pia.”

B. Kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani.”
   1. Gal.2:14-16.

**Mstari wa 21**

A. “Msishike, msionje, msiguse.”
   1. Gal.4:8-10.
   2. Rum.7:5.
   3. Gal.3:3.

**Mstari wa 22**

A. “*Hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu*.”
   1. Coffman anaandika hivi: - “Tena rejea imetolewa kwa mkuu wa Magna Carta wa dini ya Kikristo katika Injili ya Mathayo, ambamo Mwokozi anafananisha mapokeo na maagizo ya wanadamu akisema, ‘Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.”

   2. Mk.7:14-19.

Mstari wa 23

A. “*Mambo hayo yanaonekana kuwa yana hekima.*”
   1. Lakini si katika hekima itokayo juu.
      a. Yak.3:13-18.

B. “*Ibada ya kujitungia*.”
   1. Ni kinyume na ibada ambayo Mungu ameiagiza.

C. “*Katika kunyenyekea na katika kuutawala mwili*.”
   1. Kujinyima anasa za mwili, kupenda kuonekana mbele za watu.
      a. Vyote ni katika dhana za kufikirika tu.

**SURA YA TATU**

**Mstari wa 1**

A. "*Basi ikiwa mmefufuka pamoja na Kristo*.
   1. Kol.2:12; Rum.6:3,4.
   2. Efe.2:1-6.

B. "*Yatafuteni yaliyo juu*."
   1. Flp.3:20; Yoh.14:3.
   2. Math.6:19-24.
   3. Kol.2:11 – "kuufia ulimwengu."
      a. Rum.6:17,18 – "Kuwa hai katika Kristo."
   4. Ukweli ni kwamba, Wakristo hawana uhai ulio wao wenyewe. Uzima wao ni uzima wa Kristo.
      a. Flp.1:21; Gal.2:20.
   5. Efe.2:6.

C. "*Kristo aliko*."
   1. Mdo.2:30.
   2. Ufu.3:21.
   3. Mdo.7:55,56.
   4. Yeye ni kichwa chetu, Kol.1:18.

**Mstari wa 2**

A. "*Yafikirini yaliyo juu*."
   1. Amua kutenda mambo kama vile Kristo angeamua.
      a. Angalia maelezo katika mstari wa kwanza.

B. "*Siyo yaliyo katika nchi*."
   1. Malengo yenu yasifungwe katika masuala ya nchi, msitilie maanani mambo madogo na yasiyo na maana.
      a. 1 Yoh.2:15; Yak.4:4.
      b. Yoh.15:19.

**Mstari wa 3**

A. "*Kwa maana mlikufa*."
   1. Yoh.12:24,25; Rum.6:3,4; Gal.2:20; Flp.1:21.
   2. Baraka na wajukumu.

**Mstari wa 4**

A. Ni suala la kusisitiza.
   1. Tafuteni mambo yaliyo juu.
      a. Yafikirini mambo yaliyo juu.
      b. Uhai wenu umefichwa ndani ya Kristo.
      c. Kristo ndiye uhai wetu.

   2. Yoh.14:6; 6:68; 10:10.
      a. Yoh.3:5; Rum.6:3,4; 2 Kor.5:17.

   3. Flp.23:10,11.

B. "*Kristo atakapofunuliwa*."

1. Mdo.1:11; Ufu.22:20.
2. 1 Thes.4:15.
3. 2 Pet.3:9,10.

C. “*Mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu*.”
   1. Rum.8:18.

**Mstari wa 5**

A. “*Basi vifisheni viungo vyenu vilivyo katika nchi*.”
   1. Vifisheni - Mortify (Kiyunani – NEKROO) – kuviua.
      a. Rum.4:19 – Mwili wa Abrahamu “sasa umekufa” – Ebr.11:12.

   2. Kutoka Kiyunani – NEKROS.
      a. Efe.2:1.

   3. Rum.6:11.
   4. Gal.5:17.

B. Uasherati (Kiyunani – PORNEIA).
   1. Tendo lolote la kukutana kimwili kinyume na mpango wa Mungu,.
   2. Mara nyingi uasherati ulihusishwa na ibada za kipagani.
   3. Gal.5:19.

C. Uchafu (Kiyunani – AKATHARSIA)
   1. Uchafu kimaadili.
   2. Efe.4:19.
   3. Efe.4:19.

D. Tamaa mbaya (Kiyunani – PATHOS).
   1. Huba ndani ya akili, uchu mkubwa.
      a. Daima inahusu “tamaa mbaya katika Agano Jipya.”
         1) Rum.1:26; 1 Thes.4:5.

E. Mawazo mabaya (Kiyunani – EPITHUMIA).
   1. Matamanio, uchu wa kutaka.
      a. Rum.7:8; 1 Thes.4:5.

F. Kutamani (Kiyunani – PLEONEXIA).
   1. Shauku la kutaka zaidi.
   2. Daima hutumika kwa maana mbaya.
      a. Efe.5:3.
      b. Lk.12:15-21; 1 Tim.6:6-18.
   3. Ni ibada ya sanamu.

**Mstari wa 6**

A. Ghadhabu ya Mungu.
   1. Injili hutuasa juu ya mambo haya.
      a. Rum.1:16.
      b. 2 Thes.1:7-9.

2. Ufu.6:16,17; 11:22.

**Mstari wa 7**

A. "*Katika hayo ninyi nanyi mlitembea zamani.*"
   1. Efe.2:1-3.
   2. Efe.5:8.
   3. Tito 3:3.
   4. Amosi 3:3.

B. "*Mlipoishi katika hayo*."
   1. Kuna watu ambao wanasema, hauwezi kuishi katika dhambi, hasa katika uasherati.
      a. Paulo alisema, ndugu hao waliwahi kuishi katika mambo hayo.

**Mstari wa 8**

A. "*Lakini sasa yawekeni mbali nanyi hayo yote*."
   1. Kuna mambo mengine zaidi hayo aliyotaja.

B. Hasira (Kiyunani – ORGE).
   1. Hali ya kukaa au kudumu akilini kukasirika, mara nyingi kwa nia ya kulipiza kisasi.

C. Ghadhabu (Kiyunani – THUMOS).
   1. Sasa angalia tofauti kati ya "ORGE" na "THUMOS."
      a. "THUMOS" – zaidi ni hisia za ndani.
      b. "ORGE" – Zaidi ni utekelezaji wa hisia.

D. Na uovu (Kiyunani – KAKIA).
   1. Tabia mbaya – kinyume na iliyo bora.
   2. Kufikiria maovu yenye kudhuru.

E. Matukano (blasphemy) – Kiyunani - BLASPHEMIA.
   1. Katika Efe.4:31 "matukano" (evil speaking).
      a. Shutuma za kukaripia.

F. Matusi vinywani mwenu (filthy communication) – Kiyunani – AISCHROLOGIA.
   1. Angalia W.E. Vine.

**Mstari 9**

A. "*Msiambiane uongo*."
   1. Yoh.8:44; Ufu.21:8.
   2. Efe.4:25.

B. "*Mmevua utu wa kale*."
   1. Umeharibika…uliodanganywa kwa matamanio.
      a. 1 Yoh.2:15-17.
      b. Ufu.12:9.
         1) Ebr.11:25 dhidi ya Rum.6:23.

   2. Gal.5:17.

**Mstari wa 10**

A. "*Mkivaa utu umpya*."
   1. Mtu mpya huonekana kwa matendo ambayo hutiririka kutoka katika akili mpya. Mk.7:15.

B. "*Unaofanywa upya*."
   1. Efe.4:18 dhidi ya 20,21.
   2. Rum.12:1,2.
   3. Flp.4:8 na kutafakari.

C. Mfano wake Kristo.
   1. Gal.Efe.2:13-16; Mwa.1:26,27; 1 Pet.2:21.

**Mstari wa 11**

A. "*Hapo hapana Myunani wala Myahudi*."
   1. Gal.3:28.
   2. Rum.2:11; Mdo.10:23.
   3. Efe.2:13-16.
   4. Watu wote wanasimama sawa chini ya msalaba.

B. "*Bali Kristo ni yote, na katika yote*."
   1. Yeye ndiye mtangulizi wa wote.
      a. Ondoa kabisa tofauti zote.

   2. 1 Kor.10:31; Flp.1:21; Gal.2:20.

Mstari wa 12

A. "*Basi,…jivikeni*."
   1) Dini ya Kristo haitoi makatazo tu;
   2) Bali pia inabainisha mambo tunayopaswa kuyatenda.
      a) Lk.11:24-26.

B. Wateule, watakatifu, na wapendwao.
   1. Wateule.
      a. (Kiyunani – EKLEGO) – kuchagua, kuteua kimoja kubagua.

   2. Watakatifu.
      a. 1 Pet.1:13-16.
      b. Kol.1:2.

   3. Wapendwao (Kiyunani – AGAPAO).
      a. Hawa ndio walioupokea upendo wa Mungu.
         1) Yoh.3:16; Rum.5:8,9.

C. Moyo wa rehema.
   1. Moyo (bowels) – Kiyunani – SPLAGCHNON.
      a. Ushairi kwa Kiyunani.
         1) Ilitazamwa kama makao yenye mwamko usiozuilika, kama vile hasira na upendo.

      b. Waebrania.
         1) Wayahudi waliona kama makao ya upendo yenye kujaa huruma.
            a) Haswa utokapo utu wema, ukarimu, huruma.

        2) Kwa hiyo basi, moyo uliojaa rehema, huruma au masikitiko.

  2. Math.5:7; Yak.2:13.
     a. Efe.2:4; Mik.7:18.

D. Utu wema (Kiyunani – CHRESTOTES) fadhili, karimu. Neno hutoa tabia za jinsi ya kuwa mtu mwema (mpole).
  1. Kuhusu Mungu.
     a. Yona 4:2 – "…Kwa maana nalijua ya kuwa wewe u Mungu mwenye neema, umejaa huruma, si mwepesi wa hasira, u mwingi wa rehema, nawe waghairi mabaya."

     b. Efe.2:7 – "Ili katika zamani zinazokuja audhihirishe wingi wa neema yake upitao kiasi kwa wema wake kwetu sisi katika Kristo Yesu."

     c. Tito 3:4 – "Lakini wema wake Mwokozi wetu Mungu, na upendo wake."

  2. Kwetu sisi.
     a. 2 Pet.1:5-7.

E. Msimamo wenye unyenyekevu.
  1. Yak.4:10; Flp.2:1-8.
  2. Obad.3; Mitha.16:18.

F. Upole (Kiyunani – PRAOTES) kutia lijamu au kuzitia nguvu chini ya ulinzi.
  1. Math.5:5.
  2. Math.11:28,29.

G. Uvumilivu (Kiyunani – MARKROTHUMIA).
  1. Angalia maelezo katika sura 1:11.

**Mstari wa 13**

A. "*Mkichukuliana na kusameheana*."
  1. "Mkichukuliana" (ANECHO) – kustahimili, kubeba mizigo pamoja, kuvumiliana.
     a. Efe.4:2.
        1) Mwenendo wa umoja.
           a) Unyenyekevu.
           b) Upole.
           c) Uvumilivu.
           d) Kuchukuliana.

        2) Upendo ni muhimu.
           a) Kol.2:2.
           b) Rum.12:10.
           c) Yoh.13:15.
           d) 1 Pet.1:22.
           e) 1 Pet.2:17.

  2. Mkisameheana.
     a. Mik.7:18; Yona 4:2.

B. "*Mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake*."
   1. Kutakuwepo matatizo yanayoinuka kati ya ndugu.
      a. Maoni mengine:
         1) Mdo.15:39-41.

      b. Mambo mengine ni masuala ya mafundisho.
         1) 1 Kor.5 na Gal.2.

C. "*Kama Bwana alivyowasamehe ninyi*."
   1. Ni namna gani Kristo ametusamehe?
      a. Je, kuna masharti au hakuna masharti kabisa?
      b. Nia ya Kristo ilikuwa ipi?

   2. Lk.17:3; Mdo.2:38; 1 Yoh.1:9.

**Mstari wa 14**

A. "*Zaidi ya hayo yote jivikeni upendo*."
   1. Efe.5:2.
      a. Upendo ni uwezo wa utendaji.
         1) 1 Kor.16:14; 1 Thes.1:3.
         2) 1 Yoh.3:17,18.
         3) Yoh.14:15; Ufu.3:19.

      b. Pengine kupoteza nia hii.
         1) Ufu.2:1-5.

   2. Kristo alitupenda na kujitoa – Yoh.3:16; 2 Kor.8:9.

   3. Yoh.13:34; Rum.13:8; 1 Kor.13.

B. "*Kifungo cha ukamilifu*."
   1. Ukamilifu (Kiyunani – TELEIOTES) – hali ya utimilifu.
      a. Kutoka katika Kiyunani – TELEIOS) umri kamili, timilifu.

   2. Hatuwezi kuwa Wakristo waliokomaa pasipo kuvaa upendo.

**Mstari wa 15**

A. "*Na amani ya Kristo iamue mioyoni mwenu*."
   1. Amani.
      a. Isa.9:6.
      b. Lk.1:79 – "…Na kuingoza miguu yetu kwenye njia ya amani."
      c. Lk.2:14
      d. Yoh.14:27.
      e. Mdo.10:36 – Neno lile alilowapelekea wana wa Isaraeli akihubiri habari njema ya amani kwa Yesu Kristo – Rum.10:15.
      f. Mungu wa amani – Rum.15:33; 16:20; Ebr.13:20; Flp.4:9.
      g. Flp.4:7
      h. Kol.1:20; Efe.2:14-17.

2. Basi, si jambo la ajabu kwamba amani inatakiwa itawale mioyoni mwetu.

B. "*Ndiyo mliyoitiwa katika mwili mmoja*."
   1. Injili ya amani (Rum.10:15) inatuita (2 Thes.2:14).
   2. Mwili mmoja
      a. Efe.4:4; 1 Kor.12:20; Math.16:18.

C. "*Tena iweni watu wa shukrani*."
   1. Zab.75:1; Flp.4:6.
   2. 2 Kor.2:14; 1 Kor.15:57.

**Mstari wa 16**

A. "*Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu*."
   1. Yoh.12:48.
   2. Mdo.20:28; Yak.1:21; Rum.1:16; 10:17.
   3. Zabu.1:2.
   4. Zab.119:9,11.

B. "*Katika hekima yote.*"
   1. 1 Kor.1:20,21.
      a. Yak.3:13-18.
         1) Kuangalia kama vile Mungu anavyoona.

C. "*Mkifundishana na kuonyana*."
   1. Efe.5:19 – "Mkisemezana" (speaking to yourselves – KJV) – (Speakingi one to another" ASV.

   2. Kiwakilishi akisi (reflective pronoun).
      a. Ni tendo la kupeana.

      b. E.G. Sewell: "Washiriki wa kanisa wao wenyewe na kwa ajili yao ndio wanaotakiwa kuimba, na hawezi kuikabidhi kazi hii kikundi cha kwaya, kiwe chenye kinanda au pasipo kinanda."

D. "*Zaburi na nyimbo na tenzi za rohoni*."
   1. Zaburi (PSALMOS).
   2. Nyimbo (HUMNOS).
   3. Tenzi za rohoni (ODES PNEUMATIKAIS).
      a. Zaburi zinaweza kurejea kwa Zaburi za Agano Jipya.
      b. Aina hizo tatu zinaweza kurejea nyimbo za washiriki wa kanisa la kwanza, zilizoandikwa kwa uvuvio wa Roho Mtakatifu.

E. Zaburi (Psallo.)
   1. Wengine wanajaribu kusema neno hilo ni vyombo vya muziki.
   2. Hebu tuchunguze kwa makini.
      a. Tafsiri ya neno:
         1) Kugusa, kuhisi, kuamsha, au hisi kwa kugusa, hasa kuvuta nyuzi au shtusha ghafula.
         2) Kuvuta na kuachia, kuvuta nyuzi au shtua ghafula na kuachia kidole.
         3) Kwa kawaida ni nyuzi za vyombo vya muziki, kupiga chombo cha muziki ukitumia vidole, badala ya kutumia chuma cha kupigia gitaa kinachovaliwa kidoleni.

      b. Muhtasari:

1) Mtikisiko wa uzi au kamba ambayo huunda sauti.
2) Hailengi nyimbo zilizoimbwa kwa uzi wa chombo, bali sauti iliyoundwa na kamba iliyopigwa.
3) Chombo kinachotetemeka ni sauti inayotumika katika uimbaji.

g. "*Huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu*."
1. "Mkiimba" (ADONTES) - Daima limetumika sifa kwa Mungu.

2. "*Kwa neema mioyoni mwenu*."
a. Ibada yetu ni lazima akili zetu ziwe na matunda.
b. Yoh.4:24; 1 Kor.14:15; Amos 5:21ff.

3. Mbele za Bwana.
a. Ibada zetu zielekezwe kwa Yehova.
b. Math.4:10.

MAFUNZO MAALUM JUU YA MUZIKI KANISANI

A. Kanuni za kujifunza mambo tunayopaswa kuyaelewa.
1. Mamlaka.
a. Ukimya wa Maandiko (silence of the Scriptures).
1. Ebr.1:5; Mdo.15:24..22
2. Kumb.4:2; Mith.30:6; Ufu:18; 2 Yoh.9.

b. Kwa hiyo, kila jambo ni lazima tulifanye kama vile tunavyoamriwa katika Maandiko. Ikiwa hatulioni katika Maandiko, hilo hatupaswi kulifanya.

2. Lazima tuiangalie Biblia kikamilifu katika kila mada.

B. Hebu sasa na tutumie kanuni hizi katika "muziki wa kanisa."
1. Maandiko.
a. Imba – Rum.15:9; Ebr.2:12.
b. Imba Zaburi – Yak.5:13.
c. Wakamwimbia Mungu sifa – Mdo.16:25.
d. 1 Kor.14:15.
1) "Nitaimba katika roho."
2) "Nitaimba katika akili pia" (with the understanding).
e. Efe.5:19.
1) "Mkisemezana."
2) Zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni.
3) Mkiimba.
4) Kumshangilia Bwana mioyoni mwenu.
5) Tunamwimbia Bwana.

f. Kol.3:16.
1) Mkifundishana na kuonyana.
2) Zaburi, nyimbo na tenzi za rohoni.
3) Mkimwimbia Mungu.
4) Kwa neema mioyoni mwenu.
5) Zimwelekee Bwana.

2. Muhtasari:
    a. Ni lazima tuimbe – tumeruhusiwa kuimba.
    b. Ni lazima tuimbe zaburi, tenzi na nyimbo za rohoni – aina ya nyimbo tulizoamriwa.
    c. Mkisemezana ninyi kwa ninyi, mkifundishana na kuonyana – tendo la kupokezana – Wakristo ni sharti waimbe kwa kusemezana.
    d. "*Huku mkishangilia Bwana mioyoni mwenu*."
        1) Ni tendo la ufahamu utokao moyoni.
        2) Tendo la kutoa na kushirikiana.

3. Unaonaje?
    a. Vyombo vya muziki?
    b. Vipi juu ya nyimbo nyingine (polkas, za jadi, mashairi, n.k.)?
    c. Ni wapi Biblia inaamuru juu ya muda na mahali pa kuimba?

**Mstari wa 17**

A. "*Na kila mfanyalo katika tendo au neno*."
1. Maneno na matendo chimbuko lake ni moyoni.
    a. Mk.7:15.
    b. Mitha.23:7.
    c. Flp.4:8.
    d. Zab.1:2.

2. Maneno.
    a. Math.12:34-37.
    b. Zab.19:14.
    c. Yako.3.\

3. Matendo.
    a. Efe.2:10.
    b. Flp.2:12.
    c. Mdo.10:38.
    d. Yak.4:17.

B. "*Fanyeni yote katika jina la Bwana*."
1. Math.28:18,19.
2. Kristo ametangulia mbele ya vitu vyote ana mamlaka yote.
3. Kol.1:18.
4. Mdo.2;38.
5. 1 Kor.10:31.

C. "*Mkimshukuru Mungu Baba kwa yeye*."
1. Flp.4:6.
2. Zab.75:1.

UTII NA MAMLAKA

A. Hatujadili uduni au thamani ya mtu.
1. Gal.3:28.
2. 1 Pet.3:7.

B. Fafanuzi:
    1. 1 Kor.11:3.

**Mstari wa 18**

A. "Ninyi wake, watiini waume zenu."
    1. Efe.5:22.
    2. Mwa.2:23-25.
    3. Tito 2:4.

B. Kama ipendezavyo katika Bwana.
    1. 1 Kor.11:13.

**Mstari wa 19**

A. "*Ninyi waume, wapendeni wake zenu*."
    1. Upendo
        a. "EROS" – huba.
        b. "PHILA" – upendo wa ushirikiano.
        c. "AGAPE" – kujitoa mwenyewe, kujitoa dhabihu.

    2. Huu hapa ni upendo wa "Agape."
        a. 1 Yoh.3:18; 1 Thes.1:3.
        b. Yoh.3:16.

B. "*Msiwe na uchungu nao*."
    1. Kumbuka Efe.5:28-33.

**Mstari wa 20**

A. "*Ninyi watoto, watiini wazazi wenu katika mambo yote*."
    1. Efe.6:1-3.

    2. Baba yetu aliye mbinguni anatarajia utii kwetu.
        a. Math.7:21; Lk.6:46; Yoh.14:15; 14:14; Ebr.5:8,9.

    3. Daima ameamuru watoto kuwatii wazazi wao.
        a. Kumb.21:18-21.
        b. Kut.20:12.

    4. Efe.6:1 panasema "katika Bwana."
        a. Uongozi wa Mungu.
            1) Mdo.5:39.
            2) Lk.14:26,27.

B. "*Maana jambo hili lapendeza katika Bwana*."
    1. Efe.6:1.

**Mstari wa 21**

A. "*Akina baba*."
    1. Yeye ni kichwa cha familia – Efe.5:23.
    2. Kumbu.6:1-9 – uwe na heshima kama mzazi.

a. Hakika utangulize ufalme wa Mungu kwanza.
   1) Math.6:33; Mk.12:30; Flp.3:14.
   2) Lk.5:23; 14:27.

b. Kumweka baba nyuma asiwe kichwa cha nyumba.
   1) 1 Tim.5:8.
   2) Maonyo kwa watoto.

c. Kuwaweka akina mama nyuma ya nyumba.
   1) Tito 2:5.
   2) Mithali 31:25-28.

d. Nidhamu.
   1) Mambo chanya – mafunzo.
      a) Kumb.6:1-9; Mith.22:6.
      b) Kuwafundisha watoto wetu kuhusu utoto.

   2) Kurekebisha au kusahihisha.
      a) Ebr.12:5-11; Ufu.3:19.
      b) Mith.29:15,17; 13:24; 19:18; 23:13,14.

   3) Kuwa na msimamo.

   4) Mambo matatu kuhusu nidhamu.
      a) Kupenda kabla ya kutoa adhabu.
      b) Kuwa na rehema wakati wa nidhamu.
      c) Kusamehe baadaye.

B. "*Msiwachokoze watoto wenu*."
   1. Kuna maeneo ambayo hatupaswi kuridhia.
      a. Sheria za Mungu lazima zifuatwe – na watoto pia wazingatie.
      b. Kukua na kukomaa kutawafanya watoto watambue majukumu.

   2. Pili, kuna njia ya kulea ambayo inaweza kutoonyesha upande wowote (neutral).
      a. Akina baba lazima wawe makini wala wasiwe mizigo kwa watoto hata kuwakasirisha au kuwavunja mioyo.

   3. Watoto wana roho.
      a. Kushinda kuitia lijamu roho hiyo itasababisha kuipoteza utumike chini ya utumishi wa Shetani.
      b. Kuivunja kabisa roho hiyo inaweza kupoteza nguvu, juhudi na imani iliyo na thamani.

C. Fundisha, onya na toa uhuru kama vile Bwana anavyotoa uhuru kwetu. Isiwe mazoea ya kusema "hapana", kwa sababu tu ya kusema hapana.

**Mistari ya 22,23**

A. "*Watumwa na mabwana*."
   1. Biblia haipingi au kuunga mkono moja kwa moja utumwa. Lakini, hata hivyo, huhalalisha kwa namna ambayo ingeutokomeza usiwepo kabisa.

2. Sasa hebu na tuangalie mtazamo wa utumwa karne ya kwanza – "Mtumwa hakuwa bora kuliko mnyama; wazee na wagonjwa lazima watupwe nje hata wafie huko kwa njaa; mtumwa anapokuwa mgonjwa, ni uharibifu kumpatia chakula; mabwana zao wana uwezo juu ya uhai na kifo cha watumwa; Augusto aliwaua watumwa mithili ya kuua ndege wa kufugwa; kwa nguvu Polio alimtupa mtumwa chini akiwa hai katika mteremko mkali wa shimo refu katika bwawa la samaki kwa sababu tu alidondosha na kuvunja bilauri. Mke wa msomi mmoja wa Rumi alimwua mtumwa kwa sababu alipatwa na hasira tu. Watumwa waliofanya kazi kama wajakazi walichanwa shavu, walinyofolewa nywele, au kuchomwa bila huruma na chuma cha moto na mabwana zao wasio na huruma." (William Barclay, *The Letters To The Galatians And Ephesians*).

A. Watumwa.
   1. Watumishi walipaswa:
      a. Kutii.
      b. Kuwaheshimu mabwana zao, na
      c. Kutumika kwa moyo.
      d. Kama kumtumikia Bwana.
         1) Siyo utumishi wa kujionyesha kwa macho.
         2) Bali kufanya mapenzi ya Mungu toka moyoni.

   2. Kol.3:22.

   3. 1 Tim.6:1; Tito 2:9; 1 Pet.2:18.
      a. Jina na mafundisho ya Mungu yasitukanwe.
      b. Wasiwe wenye kujibu haraka au kupinga.
      c. Hata kwa bwana aliye mkali.

**Mstari wa 24**

A. "*Ujira wa urithi*."
   1. Lengo letu kubwa linatakiwa liwe kumpendeza Kristo.
      a. Yeye ni Mwokozi wetu, Mdo.4:12.
      b. Yeye ndiye aliye msingi wetu, 1 Kor.3:11.
      c. Yeye ndiye njia yetu kwenda kwa Baba, Yoh.14:6.
      d. Yeye ndiye kimbilio na nguvu yetu, Zab.46:1.
      e. Yeye ni mwamuzi wetu, 2 Tim.4:1.

   2. Kristo Yesu pia anatoa thawabu ya urithi.
      1. Efe.1:18.
      2. 1 Pet.1:4.

B. "*Mnamtumikia Yesu Kristo*" (For ye serve the Lord Christ).
   1. Tito 1:1 – mtumishi.
   2. Filemoni – mfungwa.
   3. Rum.6:17,18.
   4. Rum.12:1.
   5. Math.4:10.

**Mstari 25**

A. "*Maana adhulumuye atapata malipo ya udhalimu wake*."
   1. Kipimo ni cha haki.
      a. Rum.1:16,17 dhidi ya Rum.2:9.

2. Nahumu 1:3.
3. Nabii Habakuki.

B. Hakuna upendeleo juu ya awaye yeyote.
   1. Rum.2:11.
   2. Gal.3:28.
   3. Wanadamu wote wanasimama chini ya msalaba wakiwa sawa.

## SURA YA NNE

**Mstari wa 1**

A. "*Ninyi akina bwana…*" (masters).
   1. Paulo akishamaliza hotuba yake juu ya wajibu wa watumwa.
      a. Kama watumwa, kwa mfano Onesimo, wamekuwa na majukumu yao, kadhalika mabwana, mfano Filemoni.

   2. Angalia, hakuna amri ya kuwaachia huru.
      a. Filem.12-14 - inaweza kugusa jambo lenyewe.

   3. Efe.6:5-9.
      a. Mabwana lazima.
         1) Kutenda kulingana na sheria.
         2) Si kwa kuogofya.
         3) Wanapaswa kutambua kwamba nao pia wanaye Bwana mbinguni.
         4) Watambue kwamba kuwa mabwana hapa duniani hakuna maana yoyote mbinguni.

**Mstari wa 2**

A. "*Dumuni sana katika kuomba*."
   1. 1 Thes.5:17; Lk.18:1; Math.7:7,8.
   2. "Kesheni, mwombe msije mkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu" – Math.26:41.

B. Endelea kukesha katika mambo kama hayo.
   1. Kol.2:8; 1 Pet.5:8.
   2. Efe.6:18.

C. Pamoja na shukrani.
   1. Sala pamoja na shukrani hazitenganishwi.
      a. Flp.4:6.

**Mstari wa 3**

A. "*Mkituombea na sisi pia*."
   1. Sala ni mambo ya mtu binafsi.
      a. 1 Tim.2:1,2.

   2. 2 Thes.3:1; Rum.15:30 – Jitahidini pamoja nami katika sala zenu kwa ajili yangu.

   3. Paulo daima aliwaombea wengine.
      a. Kol.1:9.

    b. Efe.1:16.

B. "*Kwamba Mungu atufungulie mlango kwa lile neno lake, tuinene siri ya Kristo*."
  1. 2 Thes.3:1.
  2. Efe.6:19 – maombi kwa ajili yangu "nipewe usemi kwa kufumbua kinywa changu."
  3. Mlango ufunguke kwa wakati mwingine.
    a. 1 Kor.16:9 – nimefunguliwa mlango mkubwa wa kufaa sana, na wako wengi wanipingao.
    b. 2 Kor.2:12.

C. Kunena siri ya Kristo.
  1. 1:26; 2:2.
    a. Efe.3:1.

  2. Flp.1:7.

**Mstari wa 4**

A. "*Ili nidhihirike…*"
  1. 1 Kor.9:16.
  2. Apate mafanikio ya maneno yake.
    a. Mdo.14:1-2 na Efe.4:15.
    b. Yer.1:10 na 2 Tim.4:2.

  3. Yuda 22,23.

**Mstari wa 5**

A. "*Enendeni kwa hekima  mbele yao walio nje*."
  1. Efe.5:15.
    a. Jihadharini sana (circumspectly) AKRIBOS – mwenendo sahihi hutokana na kuwa mwangalifu.

  2. Hekima dhidi ya upumbavu.
    a. Yak.1:5,6; 3:17.
    b. Kol.1:9,10.
    c. 1 Kor.2:4,5.
    d. 1 Kor.1:18,20,21; 3:18,19.

B. "*Mkiukomboa wakati*."
  1. Kununua fursa.
  2. Tumia vyema wakati wote kwa kutenda mema.
  3. Efe.5:16 – "Mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu."

**Mstari wa 6**

A. "*Maneno yenu yawe na neema siku zote*."
  1. Yawe mema na yenye neema, ya kupendeza, mazuri na ya heshima.
    a. Mhub.10:12 – "Maneno ya kinywa chake mwenye hekima yana neema; bali midomo ya mpumbavu itammeza nafsi yake."
    b. Kol.3:16.
    c. Efe.4:19 (soma).

B. "*Yakikolea munyu*."

1. Mk.9:50.
    a. Miongoni mwa waandishi wa Kiyunani chumvi ilionyesha hekima ambapo mazungumzo yalisifiwa bure."
        1) Pengine – wanasheria walilitumia kama utani, au hekima.

    b. Kumbuka:
        1) Nguvu ya kuhifadhi na kutakasa (purifying).
        2) Mazungumzo yenu yawe mazuri, na wala yasiwe machafu.

C. "*Mpate kujua jinsi iwapasavyo kumjibu kila mtu."*
1. 1 Pet.3:15.
2. 2 Yak.3:1,2.

**Mstari wa 7**

A. "*Tikiko*."
1. Mtu kutoka Asia, pengine Efeso.
    a. Alikwenda pamoja na Paulo kupeleka changizo.
        1) Mdo.22:4ff; 1 Kor.16:1-4.

    b. Alichukua nyaraka kwenda Kolosai na Efeso.

    c. Pia alikuwa na kazi ya kuikamilisha katika Krete.
        1) 2 Tim.4:12; Tito.3:12.

B. Ndugu mpendwa.

C. Mtumishi mwaminifu.

D. Mjoli wangu katika Bwana.

**Mstari wa 8**

A. "*Ambaye nimemtuma*."
1. Efe.6:22.
2. Faraja yenu itatokana na kujua mambo ya Paulo.

**Mstari wa 9**

A. "*Onesmo*."
1. AWOL; mtumwa wa Filemoni. (AWOL – neno la kijeshi likimaanisha kukosa kuwepo bila ya likizo.)
2. Filemoni.

**Mstari wa 10**

A. "*Aristarko*"
1. Mdo.19:20.
2. Mdo.20:4.
3. Mdo.27:2.
4. Filem.24.

B. "*Marko, mjomba wake Barnaba*."
1. Mdo.15:37.

        a. Mdo.13:3 – Aliwaacha Perga ya Pamfilia.

    2. Marko.

    3. 2 Tim.4:11.

**Mstari wa 11**

A. "*Yesu, aitwaye Yusto*."
    1. Hakuna mtu mwingine aliyemtaja mtu huyu.

B. "*Hao peke yao ni watendaji wa kazi pamoja nami*."
    1. 1 Kor.3:6-9.

C. "*Nao walikuwa faraja kwangu*."
    1. Faraja (PAREGORIC) – kupunguza maumivu.
        a. Kwa sehemu kubwa ni dawa iliyojulikana kwa ajili ya watoto.

**Mstari wa 12**

A. "*Epafra*."
    1. Angalia maelezo katika 1:7.

B. "*Akifanya bidii siku zote kwa ajili yenu katika maombi*."
    1. Inawezekana alikuwa mwombaji mkubwa.
        a. "Mwenye kuugua kwa mateso."

C. "*Ili kwamba msimame wakamilifu na kuthibitika sana katika mapenzi yote ya Mungu*."
    1. Sisi ni walinzi wa ndugu zetu.
    2. Lazima tuwajibike katika maisha ya watu wengine.
        a. Ebr.10:24,25.
        b. Gal.6:1.
        c. 2 Tim.2:1.

**Mstari wa 13**

A. "*Maana namshuhudia…*"
    1. 1 Pet.2:17.
    2. Rum.12:10.

**Mstari wa 14**

A. "*Luka, yule tabibu mpendwa*."
    1. Mwenye kuandika Injili ya Luka na kitabu cha Matendo.
    2. Mahali hapa tu ndipo alipotajwa kuwa tabibu.
        a. Mtindo anaotumia kuandika vitabu vyake unathibitisha kuwa alikuwa tabibu.

B. Dema.
    1. Filem.24.
    2. Hapa.
    3. 2 Tim.4:10.

**Mistari ya 15,16**

A. Mambo ya kuzingatia ya mwisho.

**Mstari ya 17**

A. “*Arkipo*.”
   1. Filem.2.
      a. Wengine hudhania kwamba Arkipo pengine alikuwa mtoto wa Filemoni.

B. “*Iangalie hudma ile uliyopewa*.”
   1. 1 Tim.4:6.
   2. Majukumu ya kiroho lazima tuyatie katika vitendo.
      a. Kumbuka lengo kuu.

**Mstari wa 18**

A. “Salaam zangu Paulo…”
   1. Hitimisho linalopendeza.